SportPesa
TZS. 499,059,740
CHEZA USHINDE JACKPOT
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Baba** adaiwa kufungia familia ndani, kuiteketeza kwa moto, mwingine aua mtoto kwa shoka

UKURASA 3




# Nipashe

Alhamisi Septemba 16, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580705
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

UKURASA 11

# Samia ataka wanawake wajipange urais 2025

• **Asema** ni zamu yao kwa urais, avibeza 'vijigazeti' vinavyodai hatagombea...*Uk. 2*



## YALIYOMO

UKURASA WA 4
**SABAYA KUSOMEWA MAELEZO KESI UHUJUMU**
MKUU wa zamani wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole...

UKURASA WA 4
**MABASI YAFUNGWA KAMBA, NAILONI KWA BREKI**
JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani nchini kimefanya...

UKURASA WA 9
**MAGONJWA YANAVYOUA MIFUGO MINGI MEATU**
WAFUGAJI wa Wilaya ya Meatu mkoani Simiyu wanaopakana na...

# Uhaba wa maji kuikumba D' Salaam

UKURASA 3



Wakili anayemtetea Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe (kulia) na wenzake, Peter Kibatala, akizungumza na wateja wake, baada ya kufikishwa katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, mkoani Dar es Salaam jana, kusikiliza kesi inayowakabili ya uhujumu uchumi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ushahidi RPC waibua mvutano kesi ya Mbowe

UK. 2

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA
ISO 9001: 2015 Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga
TMA

TANGAZO KWA UMMA

KIBALI KWA SHUGHULI ZA UANGAZI NA USAJILI WA VITUO VYA HALI YA HEWA KWA MUJIBU WA SHERIA

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) inapenda kuwataarifu wadau wote kuwa, kwa mujibu wa sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Na. 2 ya mwaka 2019, imepewa jukumu la kudhibiti shughuli za hali ya hewa nchini.

Kwa tangazo hili Mamlaka inawakumbusha kuwa, mdau anayefanya shughuli za uangazi wa hali ya hewa anapaswa kutambuliwa kwa kupewa kibali cha kufanya shughuli hizo. Aidha, mdau anayemiliki kituo cha hali ya hewa anatakiwa kuhakikisha kituo hicho kimesajiliwa.

Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.

Imetolewa Na:
MKURUGENZI MKUU
Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA)
Ubungo Plaza
Barabara ya Morogoro
S.L.P 3056
DAR ES SALAAM
TANZANIA

022-2460706/8
www.meteo.go.tz
met@meteo.go.tz

@tmaservices @tma_services @tanzaniameteorological
tanzaniametagency www.meteotz1950.blogspot.com TMAonline TV

# Samia ataka wanawake wajipange urais 2025

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan amewataka wanawake kujipanga kuhakikisha wanaweka Rais mwanamke katika Uchaguzi Mkuu ujao.

Vilevile, amehoji kilichoandikwa na moja ya gazeti nchi kwamba hana nia ya kuwania urais mwaka 2025, akiuliza 'nani kawaambia?'

Rais Samia alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam katika maadhimisho ya Siku ya Demokrasia Duniani yaliyohudhuriwa na taasisi mbalimbali na wasichana 50 ambao waliokolewa kwenye biashara ya usafirishaji wa binadamu.

Katika maadhimisho hayo, Rais Samia alikabidhiwa tuzo tatu, moja ikitolewa na Mwenyekiti wa Azaki ya Wanawake Tanzania (Ulingo), Anna Abdallah, ya pili kutoka kwa watoto waliookolewa katika udhalilishaji wa kimaisha na nyingine kutoka kwa masista wa St. Joseph.

Akizungumza katika maadhimisho hayo, Rais Samia alisema, "Leo (jana) mmempa tuzo Rais wenu, Rais mwanamke, kwa bashasha na furaha kubwa, lakini ninataka niwaambie wanawake bado hatujaweka Rais mwanamke." Mkuu wa Nchi huyo alifafanua kuwa Rais huyo mwanamke amekaa kwa sababu ya kudra ya Mwenyezi Mungu na matakwa ya Katiba.

"Tulichokichangia sisi na dada zetu na mama zetu na Mama Anna Abdallah ni ile kusukuma mpaka mwanamke akawa Makamu wa Rais, ule ndio mchango mkubwa ambao tumeufanya wanawake.

"Kama isingekuwa mpango wa Mungu, ingekuwa ngumu, tungefikia hapo kila mwaka tunakwenda ni hapo, ni hapo," alisema.

Rais Samia aliwaeleza kuwa Rais mwanamke watamweka mwaka 2025.

"Mwaka 2025 wanawake tukifanya vitu vyetu vizuri, kushikamana, tukimweka Rais wetu, tutakutana hapa kwa furaha kubwa sana. Wameanza kutuchokoza, wameanza kutuchokoza kuandika kwenye vigazeti 'Samia hatasimama', nani kawaambia?

"Fadhila za Mungu zikija mikononi kwako usiziachie, hizi ni fadhila za Mungu ndugu zangu, wanawake tumefanya kazi kubwa kuleta uhuru wa nchi hizi, wanawake tumefanya kazi kubwa kujenga siasa za nchi, tumebeba sana wanaume katika siasa za nchi hizi. "Leo Mungu ametupa baraka mikononi, tukiiachia Mungu atatulaani," alisema huku ukumbi ukilipuka kwa shangwe na kushuhudiwa waliohudhuria wakiimba 'tuna imani na mama Samia... oya... oya... oya, kweli... kweli... kweli... Samia'.

Machi 19, mwaka huu, Samia ambaye alikuwa Makamu wa Rais, aliapishwa kuwa Rais wa nchi kutokana na kifo cha Rais wa Awamu ya Tano, Dk. John Magufuli, suala hilo lilifanyika kwa mujibu wa Katiba.

Akizungumzia malengo endelevu ambayo mengi yamefanyiwa kazi, Rais Samia alisema suala la usawa wa jinsia ni miongoni mwake na kuahidi katika serikali yake wataendelea kusikia wanawake zaidi wanaingia serikalini kwa sababu anajua asipofanya, hakuna atakayekuja kulifanya. "Kwa hiyo ndugu zangu kipindi hiki ambacho Mungu ameturuzuku ndio hapa hapa, tukianza hapa atakayekuja akivuruga huo mfumo tutakuja kumsuta, sasa bora tuanze waje waguse watuone sisi ni nani, kwa hiyo ni hapa hapa mtaendelea kusikia wengi zaidi wanaingia.

"Lakini, niseme na nishukuru sana Ulingo na taasisi hizi zimeniahidi kunipa kanzidata ya wanawake ambao tunaweza kuwatumia, ni ukweli kwamba ninapopanga hizi nafasi ninapata shida sana kupata wanawake.

"Siyo kwamba hawapo, wapo lakini nikienda kwenye sifa na vigezo wengi wanadondoka, nikipata kanzidata nitakuwa na wengi zaidi, nitakuwa ninawapeleka kwenye sifa na vigezo," alihidi. Kuhusu demokrasia, Rais alisema hiyo ni dhana pana iliyobeba tafsiri nyingi ikihusisha mambo makubwa manne ambayo ni uhuru katika nchi, kuheshimu haki za binadamu, utawala wa sheria na ushiriki wa wananchi katika kuiweka serikali kupitia uchaguzi huru na wa haki.

Alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoongoza kwa kufuata misingi ya demokrasia.

Mkurugenzi wa Mawasiliano, Itifaki na Mambo ya Nje, John Mrema, akizungumzia kauli hiyo ya jana ya Rais Samia, alisema huenda ikaibua hisia kwamba Chama Cha Mapinduzi (CCM) tayari kimeshapata mgombea urais hata kabla ya kufanyika kwa vikao vya chama vya uteuzi wa wagombea wa nafasi hiyo. Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (TAMWA), Joyce Shebe, alisema uwapo wa Rais Samia Ikulu unatafsiri kuwa wanawake wanaweza na kwa sasa anaangaliwa kama mfano.

"Tungependa kuona wanawake wengi wanateuliwa ili kuweka vyema hiyo tafsiri ya wanawake wanaweza. Sasa kwa kuwa yeye yuko juu afanye yeye, lazima aonyeshe mfano anajua chini alikotoka, anajua changamoto alizopitia, aonyeshe mfano wa kuteua wanawake na itasaidia kuleta picha nzuri na jamii itajifunza kuondoa mitazamo hasi.

"Wanaoteuliwa lazima waonyeshe wanaweza, hadi sasa hatujaweka shaka kwenye wanawake aliowateua kwa kuwa wote wamefanya vyema, tunategemea hawatamwangusha na hawatawaangusha Watanzania, wakiharibu wajue italeta shaka na hatutaaminika kwamba tukipewa nafasi hatuwezi bali ni watu wa kukaa nyumbani kuosha vyombo na kulea watoto," alisema.

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI NA. 77 YA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**ASTERIA NICHOLAS MANYAKA**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**JERROLD GWASEKO**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji/mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 5 Mwezi wa 10, 2021.

Imewasilishwa Dar es salaam, leo **tarehe 13 Mwezi wa 10, 2021.**

---

# Ushahidi RPC waibua mvutano kesi ya Mbowe

**Na Kulwa Mzee**

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, Kamishna wa Polisi Msaidizi Ramadhan Kingai, amedai alimsikia Luteni Denis Urio akisema mbele ya aliyekuwa Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai (DCI), Robert Boaz, kwamba kuna kundi la kihalifu linaandaliwa na Freeman Mbowe.

Ushahidi huo wa Kingai umeibua kesi ndogo ndani ya kesi kubwa baada ya Wakili Peter Kibatala kupinga maelezo ya mshtakiwa Adamu Kasekwa kupokewa kama kielelezo mahakamani kwa madai aliteswa kabla na wakati wa kuchukuliwa maelezo hayo.

Hayo yaliibuka jana wakati Kingai ambaye ni shahidi wa kwanza Upande wa Mashtaka, alipotoa ushahidi Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi kwa kuongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Robert Kidando, mbele ya Jaji Mustapher Siyani.

Alidai alipigiwa simu na Kamishna Boaz afike ofisini kwake na alipofika, alimkuta akiwa Luteni Urio, akatambulishwa na kuambiwa ana taarifa muhimu ya kihalifu.

Shahidi huyo alidai kuwa Kamishna Boaz alimwambia Urio aeleze wakiwa pamoja na alieleza kwamba kuna kundi la kihalifu linaandaliwa na Mbowe likiwa na lengo la kuwadhuru viongozi wa serikali, kulipua vituo vya mafuta, masoko, kukata miti kwenye barabara kubwa kuzuia magari na kupora watu.

Alidai Luteni Urio aliwaambia lengo la kundi hilo ni kuifanya nchi isitawalike katika kipindi cha kuelekea Uchaguzi Mkuu.

"Denis alisema taarifa hizo aliambiwa na Mbowe, alimwambia kwa vyovyote vile atachukua mamlaka ya nchi, akamwahidi kumpa nafasi ya juu.

"Alieleza kwamba Mbowe alitaka amtafutie vijana, wawe makomandoo waliofukuzwa au kustaafu kazi, vitendo hivyo walipanga kufanya Moshi, Arusha, Dar es Salaam, Mbeya na Mwanza," alidai Kingai. Shahidi huyo alidai walipanga miti ikatwe katika Barabara ya Morogoro kuelekea Iringa na baada ya taarifa hiyo Kamishna Boaz alimshauri Urio aendelee, lakini asaidie kutoa taarifa kwake.

Alidai aliendelea kuwasiliana na Urio na kuna kipindi akamwambia vijana wamepatikana ambao ni Halfani Bwire ambaye baadaye alikuwa mlinzi wa Mbowe na Moses Jenje na Agosti 4, 2020 aliambiwa na Urio kuwa aliwapata vijana wengine wawili; Adamu Kasekwa na Mohammed Ling'wenya.

Kingai alidai Urio alimjulisha kuwa tayari vijana walishafika Moshi kwa ajili ya kumdhuru Lengai Ole Sabaya na alikwenda na kikosi chake kwa ajili ya kuweka mikakati ya kuwakamata kabla ya madhara yoyote.

Alidai walikwenda Moshi Agosti 4, 2020 na Agosti 5, mwaka huo walifanikiwa kuwakamata Adamu na Ling'wenya na walipowapekuwa Adamu alikutwa na pisto mgongoni yenye risasi tatu, kete 58 za heroine na Ling'wenya alikutwa na kete 25 za heroine na kwamba wakati wa upekuzi walikuwapo mashahidi wawili; Anitha na Esther.

Shahidi huyo alidai waliendelea kumtafuta Moses, lakini hawakufanikiwa kumpata hivyo walielekezwa kuwapeleka watuhumiwa Dar es Salaam na Agosti 7, 2020 alfajiri wakifika Kituo Kikuu cha Polisi na kuanzia saa moja na nusu hadi saa tatu asubuhi alimhoji Adamu ambaye alitia saini maelezo yake, akikiri kubali kuhojiwa akiwa peke yake.

Kingai aliomba kuyatoa maelezo hayo mahakamani kama kielelezo, lakini Wakili wa Utetezi, Kibatala alipinga yasipokewe kwa sababu mbili; yalichukuliwa zaidi ya saa nne na sababu ya pili mshtakiwa aliteswa na mchakato huo ulisimamiwa na Kingai.

Akisaidiana na Wakili Jeremiah Mtobesya, waliiomba mahakama iridhie kufanya kesi ndogo ndani ya kesi kubwa ili kusikiliza ushahidi wa mshtakiwa alivyoteswa. Upande wa Jamhuri haukupinga hilo na mahakama iliahirisha kwa muda kisha iliendelea kusikiliza kesi ndogo ndani ya kesi kubwa.

Mahakama ilikubali kuendesha kesi ndogo na Upande wa Jamhuri ulidai una mashahidi saba, lakini kwa jana ulikuwa na shahidi mmoja ambaye ni Kingai.

Kingai, akitoa ushahidi katika kesi ndogo, alidai si kweli kwamba mshtakiwa aliteswa na hakukuwa na sababu ya kufanya hivyo kwa sababu hakukuwa na ugumu katika kuwakamata.

Alidai wakiwa katika safari ya kuwaleta Dar es Salaam, hakukuwa na shida na mshtakiwa alichukuliwa maelezo akiwa hana tatizo la kiafya na alikubali kuchukuliwa maelezo akiwa peke yake.

Wakili Kibatala alimhoji shahidi endapo alieleza kama alimwambia mshtakiwa haki zake wakati wa ukamataji ikiwamo kujitambulisha na kumweleza makosa yake.

Shahidi alidai hakuongozwa na wakili kueleza hayo.

Pia alidai hakueleza mahakamani kuwa kuna wakati walimpa huduma ya chakula mshtakiwa na aliongeza kwamba mshtakiwa alimweleza ana tatizo la afya ya akili na tatizo hilo alipata akiwa kazini, lakini hakufatilia maelezo hayo.

Alihojiwa kuhusu kesi ya dawa za kulevya zinazodaiwa walikutwa nazo washtakiwa imeishia wapi, alijibu hafahamu kesi hiyo imeishia wapi.

Alidai hakusema kama mshtakiwa alikwenda Polisi Mbweni na alichokifanya akitokea Kituo Kikuu cha Polisi wakati maeneo ya katikati kuna vituo vingine.

Wakili Jeremiah Mtobesya aliendelea kuhoji, shahidi alidai alichukua maelezo ya mshtakiwa, alitia saini na kuthibitisha.

Baada ya Upande wa Utetezi kumaliza kumhoji shahidi, upande wa Jamhuri uliomba kesi iahirishwe hadi leo kwa ajili ya kuendelea kumhoji shahidi huyo pamoja na kuendelea na shahidi wa pili.

Mahakama ilikubali kuahirisha kesi hadi leo saa nne asubuhi.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, komandoo, Halfan Bwire, Adam Kasekwa, maarufu Adamu na Mohamed Ling'wenya, ambao wanakabiliwa na mashtaka sita.

## Watatu wafa kwa kuchomwa moto kisa ugomvi wanandoa

**Na Idda Mushi,** ULANGA

WATU watatu wa familia moja wamefariki dunia na mwingine mmoja kujeruhiwa baada ya nyumba waliyokuwa wakiishi kudaiwa kufungwa kwa nje na kuchomwa moto katika Kitongoji cha Ngajima, Kijiji cha Kivukoni, Kata ya Minepa wilayani Ulanga mkoani Morogoro.

Muuguzi Mkuu wa Hospitali ya Rufani ya St. Francis Ifakara ilikopelekwa miili na majeruhi wa ajali hiyo, Meshack Lubeleje, alikiri kupokea majeruhi wanne wa moto na kati yao watatu walikuwa na hali mbaya.

"Usiku wa Septemba 10 tulipokea majeruhi wanne wa ajali ya moto kutoka Kitongoji cha Ngajima mpakani mwa wilaya za Ulanga na Kilombero ambao kati yao watatu walikuwa mahututi," alisema Lubeleje.

Aliwataja waliopokewa kuwa ni Jasmine Mpoyoka, Shadya Mpoyoka, Sophia Manandele waliolazwa wadi za wagonjwa mahututi na Sheila Mpoyoka aliyelazwa wadi ya kawaida na anaendelea vizuri.

Muuguzi huyo alisema kuwa licha ya jitihada za madaktari na wauguzi kuwapatia huduma majeruhi hao, watatu kati yao walipoteza maisha Jasmine Mpoyoka na Sophia Manandele walipoteza maisha Septemba 12 kwa nyakati tofauti, huku Shadya Mpoyoka akifariki dunia Septemba 14 majira ya jioni.

Baadhi ya Ndugu wa Marehemu hao, wakiwamo Modhat Mubaraka na Twahili Mpoyoka, walidai wanahisi ajali hiyo huenda ilitengenezwa kwa makusudi na aliyekuwa mume wa marehemu Jasmine (jina tunalihifadhi).

Walidai kuwa mume alikuwa akituma ujumbe wa simu wenye vitisho kwa ndugu wa Jasmine, akidai angefanya tukio kubwa zaidi ya hilo alilofanya.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Ngajima, Antony Mtega, alisema kuwa awali Jasmine na mumewe huyo ambaye ni mwenyeji wa Mafinga mkoani Iringa, waliokuwa wanaishi Morogoro, walikuwa na ugomvi, hali iliyomfanya Jasmine kuamua kurudi nyumbani kwao kitongoji huko.

Mtega alidai Jasmine alikuwa katika hatua za kutaka kuachana na mume wake kwa kufuata taratibu za dini ya Kiislamu, jambo ambalo mume huyo awali alikubali lakini baadaye alikataa na wanaamini ndicho chanzo cha kufanya uhalifu huo.

"Mtuhumiwa anapatikana kwa namba 074... (alitaja namba za simu) na ukimpigia simu anakiri kuwa ndiye aliyefanya tukio, ni vizuri polisi wamfuatilie na kumkamata kabla hajachukua hatua zaidi," alidai mmoja wa wananchi walioshuhudia tukio hilo wilayani Ulanga.

Jitihada za kumpata Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Fortunatus Musilim, kuzungumzia tukio hili hazikuzaa matunda baada ya awali kumwomba mwandishi ampe muda kufuatilia na baadaye kudai alikuwa kwenye msiba.

# Adaiwa kumuua mtoto wake kwa kumkatakata na shoka

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

VIOLET Chaula (30) mkazi wa kijiji cha Mkongomi, Kata ya Kidugala, Wanging'ombe mkoani Njombe, anashikiliwa na polisi kwa tuhuma za kumuua mtoto wake wa kumzaa, Azgad Kinyunyu (3) kwa kumkatakata na shoka kichwani.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Hamisi Issah, alisema kwa mujibu wa maelezo ya wanandugu mwanamke huyo alikuwa na matatizo ya akili.

Alisema miezi michache iliyopita, mwanamke huyo akiwa mjini Makambako alikokuwa ameolewa, alipatwa na matatizo ya akili na kurudishwa nyumbani kwa wazazi wake ili apatiwe matibabu. Kamanda alisema akiwa na mtoto huyo ambaye alionekana kudeka, mama yake huyo aliona kuwa ni usumbufu, hivyo alichukua shoka ili kumkata kata.

"Huo ni ukatili tunaita ingawa huyu mama ni mgonjwa. Lakini sasa sheria haisemi namna hiyo," alisema Issah.

Alisema mwanamke huyo anashikiliwa na jeshi hilo na wanasubiri kukamilika kwa baadhi ya ushahidi ili afikishwe mahakamani.

Wakati huo huo, mwanafunzi wa kidato cha sita Shule ya Sekondari Mwakavuta, wilayani Makete, Ndenja Ng'wale, amejinyonga kwa kutumia kamba za manila katika mtaa wa SIDO Njombe mjini.

Kamanda Issah alisema mwanafunzi huyo alirudi nyumbani kwa ruhusa kutoka shule aliyokuwa anasoma kutokana na kuumwa jino.

Alisema alikwenda kwa shangazi yake kwa lengo la kupata matibabu, lakini katika hali isiyo ya kawaida, kijana huyo alipona jino na kuanza kuumwa na tumbo huku akitapika.

"Hapo kijana hata hatujui msongo wa namna gani ulimpata kwani alichukua sturi na kamba ya manila na kujinyonga kwenye kenchi ya nyumba hiyo hadi kufa," alisema Issah.

Alisema matukio ya kujinyonga hadi kufa familia zinapaswa kuwaangalia watu wao na kuwapa ushauri nasaha ili wasifanye vitendo hivyo.



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu mkopo nafuu wa fedha Sh. trilioni 1.3 zitakavyotumika kwenye sekta tofauti nchini. Kulia ni Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) nchini, Jens Reinke. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Uhaba wa maji sasa kuikumba Dar

**Na Frank Monyo**

BODI ya Bonde la Wami/Ruvu imesitisha kutoa vibali vipya vya uvunaji maji katika bonde hilo pamoja na kuwataka wananchi kuacha mara moja kufanya shughuli za kibinadamu kwenye vyanzo vya mito.

Hatua hiyo imekuja baada ya kupungua kwa kina cha maji, katika chanzo hicho kufuatia upungufu wa mvua kwa msimu huu na ujao pamoja na kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu.

Kaimu Mkurugenzi wa Bonde la Wami/Ruvu, Elibariki Mmasi, akizungumza na waandishi wa habari jana baada ya kutembelea chanzo hicho, alisema kina cha maji kimepungua kulinganishwa na Septemba mwaka jana, kilipokuwa na kina cha milimita 12,500 hadi kufikia 7,500 kwa sasa.

Alisema Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) inachukua milimita 5,000 kwa sekunde kutoka katika mto huo na kusisitiza kuwa kama hali ya ukame ikiendelea hivyo, mto huo utakauka na kusababisha mitambo ya DAWASA kupungua uwezo wa uzalishaji maji na kuhudumia wakazi wa Dar es Salaam na Pwani.

Alisema hivi sasa DAWASA na wateja wengine wanaotumia maji ya mto huo katika juhudi za kuhakikisha mitambo yao inakuwa na maji wanatumia mifuko ya sandarusi, maarufu viroba, kuongoza maji kwenda kwenye mitambo yao ili kukabiliana na upungufu huo.

DAWASA kwa kiasi kikubwa wanategemea maji kutoka mto huo kuhudumia wateja wake majumbani pamoja na viwanda vikubwa na vidogo vya Dar es Salaam na Pwani kutumia maji ya mto huo.

"Kuna kampuni nyingi zimekuja kwetu kuomba kibali cha matumizi ya maji, tumekataa kwa ajili ya kuyalinda maji, kwa ajili ya watumiaji wa maji majumbani hata kama ni kidogo.

Pia tumesitisha shughuli zote za umwagiliaji kwani uwezo wa mto wetu hauwezi kukidhi shughuli hiyo, tumewashauri wajenge visima, kwa ajili ya kumwagilia katika kipindi hiki cha kiangazi.

"Bodi ya Bonde la Wami/Ruvu haiwezi kuruhusu kuendelea shughuli za kibinadamu wakati mazingira ya kulinda vyanzo vya maji tumewawekea shughuli mbadala ambazo watu wanaweza kufanya katika kipindi cha kiangazi kama ufugaji nyuki, kwa hali hiyo hakuna kibali chochote kitakachotolewa kwa sasa, ili kuchukua tahadhari siku zijazo," alisema Mmasi.

Alisema bodi hiyo itaanza operesheni kali ya kubaini watu au kampuni, ambazo zinatumia maji ya mto huo bila kuwa na kibali na kuwachukulia hatua za kisheria, ili kudhibiti hali hiyo. Kaimu Mkurugenzi huyo aliongeza kuwa kilichobaki kwa sasa ni mategemeo ya mvua kunyesha mapema lakini ikichelewa, wananchi wa Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani watapata maji kidogo.

Alifafanua kuwa shughuli inayofanyika kwa sasa na bonde hilo ni kudhibiti maji kutoka katika chanzo hicho kwa baadhi ya mito kuchepushwa ovyo pamoja na ujenzi wa Bwawa la Dunda, ambalo kukitokea uhaba wa maji, litakuwa linatumiika.

"Utunzaji wa vyanzo vya maji ni jukumu la wote kwani kuacha vyanzo hivyo vitatumika kiholela madhara yake ni makubwa sana.

"Kuna faini zipo kutokana na sheria zilizowekwa katika utunzaji wa vyanzo maji kuanzia laki tatu (300,000/-) hadi Sh. milioni 50 na baada ya hapo kufunguliwa mashtaka mahakamani," alionya.

Kaimu Mkurugenzi huyo alitoa rai kwa wananchi hususani wa Dar es Salaam na Pwani kutumia maji kwa uangalifu ili kukabiliana adha hiyo.

Mwezi huu Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) imetoa tahadhari ya kuwapo ukame katika mikoa inayopata mvua mara mbili kwa mwaka, hali iliyotokea pia mwaka 2005, yaani miaka 16 iliyopita.

Mkurugenzi wa Huduma za Utabiri wa TMA, Dk. Hamza Kabelwa, alisema mifumo ya hali ya hewa inayotumika kuangalia mwenendo wa hali ya hewa imeonyesha kuwapo kwa kiwango kidogo cha mvua mpaka chini ya wastani kwa maeneo hayo.

Aliitaja mikoa inayotarajiwa kuwa na upungufu wa mvua kuwa ni Dar es Salaam, Morogoro, Tanga, Pwani katika kisiwa cha Mafia, Unguja na Pemba.


**NOTISI/TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

**MAS & ASSOCIATES CO. LIMITED & COURT BROKER**

KWA IDHINI TULIYOPEWA NA **NATIONAL BANK OF COMMERCE (NBC)** TUNATOA NOTISI YA SIKU KUMI NA NNE (14) KUANZIA TAREHE LILILOTOKA TANGAZO HILI UWE UMELIPA DENI LAKO KAMA HAUTALIPA NDANI YA MUDA TULIOKUPA TUTAUZA NYUMBA KWA NJIA YA MNADA WA HADHARA ILI KUFIDIA DENI LOTE UNALODAIWA NA **NATIONAL BANK OF COMMERCE (NBC).**

| NO | JINA | MALI ILIYOWEKWA DHAMANA | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1. | STEPHEN ELIKUNDA MTINDI | CT NO.23898-MBYLR, LO NO.379062, PLOT NO.192, BLOCK "TT" LUWAWASI / MKUZO AREA, SONGEA MUNICIPALITY I.N.O. ADEN BAHATI | KUANZIA SAA NNE KAMILI ASUBUHI (04:00) |
| 2. | JOHN CHARLES MWELI | CT NO.13459-DLR, L.O. NO. 161048, PLOT NO. 29 BLOCK '13' WEST CHINANGALI DODOMA MUNICIPALITY INO CHARLES JOHN | KUANZIA SAA NNE KAMILI ASUBUHI (04:00) |

**MASHARTI YA MNADA:**

- UKAGUZI UNAANZA MARA BAADA YA TANGAZO HILI, MASHARTI YA MNADA:
- MNUNUZI ANATAKIWA KULIPIA ASILIMIA 25% SIKU YA MNADA NA ASILIMIA 75% SIKU KUMI NA NNE (14) TOKA SIKU YA MNADA NA HUKIKOSA KULIPA MNADA UTARUDIWA NA FEDHA ULIZOLIPA HAZITARUDISHWA.
- GHARAMA ZA KUBADILISHA JINA ZA MALI NI ZA MNUNUZI MWENYEWE
- MTEJA ATATAKIWA KULIPA FEDHA TASLIM SIO HUNDI.

**KWA MAWASILIANO**
**MAS & ASSOCIATES COMPANY LIMITED & COURT BROKER**
**SIMU: 0712 667989**
**WOTE/ MNAKARIBISWA**

## Mabasi ya abiria yafungwa kamba na nailoni katika mfumo wa breki

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani nchini kimefanya operesheni maalum ya ukaguzi wa magari katika eneo la Mikumi, wilayani Kilosa, barabara kuu ya Morogoro-Iringa na kubaini baadhi ya magari madogo ya abiria kufungwa kamba ya nailoni kwenye mifumo ya breki.

Operesheni hiyo imeongozwa na Mkuu wa Usalama Barabarani nchini, SACP Wilbroad Mutafungwa na kubaini magari mabovu yanayoendelea kubeba abiria, mwendo kasi na uharibifu wa mfumo wa kudhibiti mwendo kasi.

Jumla ya mabasi ya abiria 29 na malori 10 yanayofanya safari zake Nyanda za Juu Kusini ikihusisha mikoa ya Mbeya, Njombe, Songwe, Iringa na Ruvuma, yamekaguliwa na baadhi yamekutwa yamefungwa nailoni kwenye mfumo wa breki, madereva 24 wakitiwa mbaroni na kulipa faini na wengine kuzuiwa leseni zao.

Kamanda Mutafungwa na askari wa Mikumi, waliwakamata madereva wanne ambao mabasi yao yaligundulika kutosoma kwenye mfumo uliofungwa katika magari wa kudhibiti mwenendo wa magari barabarani sambamba na kupoteza kumbukumbu ili usitoe taarifa za mienendo yao pindi wanapoendesha kwa kasi.

"Madereva hawa wawekwe mahabusu kwa kuharibu mifumo inayotambua mwendokasi, madereva wengine 12 wamegungulika kuwa na makosa mbalimbali ya usalama barabarani ikiwamo ya kuendesha mabasi yao kwa mwendo kasi wa kilomita 85 hadi 89 kwa saa na hawa walipishwa faini na kuonywa," alisema SACP Mutafungwa. Pia, madereva wengine 12 walioendesha mabasi yao kuzidi mwendo wa kilomita 90 na kuendelea kwa saa, leseni zao zimezuiwa kwa hatua zaidi za kisheria.

Katika operesheni hiyo malori 10 yalikaguliwa na matano kati yake yalibainika kuwa ni mabovu kwenye mifumo ya breki hivyo kuamriwa kuyatengeneza, yakaguliwe upya ndiyo yaruhusiwe kurudi barabarani kuendelea na safari. Aidha, mabasi madogo matano yalikaguliwa na kati yake mawili yalibainika kuwa mabovu kwenye mfumo wa breki na usukani na kuzuiwa kuendelea na safari baada ya gundulika pia kufungwa kamba na mpira.

Mkuu huyo wa usalama barabarani nchini, aliwataka abiria kuwa wa kwanza kutoa taarifa kwa kikosi cha usalama barabarani wakati wote wanapoona dereva wa basi alilopanda anakiuka sheria na taratibu za usalama barabarani ikiwamo kuendesha kwa kasi ama basi husika kuwa bovu.

"Oneni ubovu wa hili gari mlilopanda, msifumbie macho, tumeni meseji (ujumbe mfupi wa maneno) au kupiga simu kwa makamanda wa usalama barabarani ambao wapo kila mahali na namba hizi zipo kwenye mabasi yote ya abiria au mkifika kwenye vituo kuna askari, toeni taarifa," alisema Mutafungwa huku akiwaonyesha picha zilizochukuliwa na askari baada ya ukaguzi wa gari walilopanda.

Aliwataka askari wa usalama barabarani nchini kufanya kazi zao kwa weledi ili kudhibiti makosa yanayofanywa na madereva wa magari ili kuepusha ajali.

Kikosi cha Usalama Barabarani nchini kimeendelea na doria, operesheni na ukaguzi mbalimbali wa magari usiku na mchana kwa vyombo vya usafiri ili kuhakikisha usalama kwa abiria na vyombo wanavyotumia.

# Chongolo ahamasisha elimu ushiriki sensa

**Na Beatrice Shayo,** LINDI

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amewataka viongozi wa chama hicho kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kushiriki katika sensa itakayofanyika Agosti mwakani, ili wapate fursa ya kupata maendeleo.

Aliyasema hayo jana wakati wa mapokezi ya ziara ya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa inayofanyika katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Njombe na Ruvuma.

Alisema serikali ina utaratibu wa kufanya sensa kila baada ya miaka 10, ili kupata takwimu ya watu na maendeleo yaweze kuwafikia.

Akifafanua alisema katika nchi hakuna maendeleo bila kufanya sensa na kwamba ni wajibu kwa viongozi kuwahamasisha wananchi ili wapate maendeleo kwa wakati.

"Serikali inapotaka kupeleka vituo vya afya katika kata kigezo cha kwanza inaangalia ni wapi kwenye watu wengi ili kupunguza madhara kwa kundi kubwa kuliko jingine hivyo kama hawatahesabiwa wananchi wanajipa fursa za maendeleo," alisema.

Aliwataka viongozi hao kurudi katika maeneo yao kufanya maandalizi ya sensa ya mwakani kwa kuwahamasisha wananchi kushiriki.

**AWAGEUKIA WANAONYEMELEA UBUNGE**

Alisema walifanya uchunguzi na kubaini bado Lindi ina changamoto ya uhusiano na tatizo lipo kwa watu wenye nafasi za juu.

"Ni lazima tubadilike sasa kwenye chama shida ni ipi? Uchaguzi umeisha mwaka jana bado kuna mtu ana ndoto ya nafasi? Tuna uchaguzi mwingine wa ndani mwakani mnagombana na watu walioenda kwenye dola kufuata nini? Mnagombea nini?" Alihoji.

Aidha, Chongolo alisema CCM ina mifumo kazi yake ni kuhakikisha inaongoza ama kutoa uongozi na kuwataka wabunge na madiwani kuendelea kufanya kazi na chama kwa kuwa kipo kwa ajili ya kuwalinda wote waliopewa dhamana.

Alisema kuna wilaya moja alikwenda na kukuta figisu kwa mbunge ambaye kila akifika anazuiliwa kutekeleza kazi za jimbo matokeo yake maendeleo hayaendi mbele.

**VIKAO VYA SHINA**

Aliagiza kufanyika kwa vikao kwenye mashina ili kusaidia kutatua kero za wananchi.

Alisema mambo makubwa wanayofanya ni kuwapongeza kwa kazi kubwa wanayoifanya ikiwamo kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka jana na serikali za mitaa.

Naye Katibu wa CCM Mkoa wa Lindi, Innocent Nanzaba, alisema wana changamoto ya maofisa ugavi hawana uelewa wa masuala ya korosho, wimbi kubwa la mifugo, barabara mbovu na kukosekana kwa mawasiliano katika baadhi ya maeneo.

Alisema wanamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kusikiliza kilio cha wananchi kuhusu tozo za miamala.



Rais Samia Suluhu Hassan akipokea tuzo kama kiashiria cha Ushindi wa Mwanamke Mtanzania, kutoka kwa Mwenyekiti wa Azaki ya Tanzania Women Cross-Party Platform/ ULINGO, Mama Anna Abdallah, kabla ya kuhutubia katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Demokrasia Duniani, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Sabaya kusomewa maelezo ya awali kesi uhujumu uchumi

**Na Allan Isack, ARUSHA**

MKUU wa zamani wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, leo anatarajiwa kusomewa maelezo ya awali katika kesi ya uhujumu uchumi namba 27.

Sabaya na wenzake sita watasomewa maelezo hayo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha.

Washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka matano ya matumizi mabaya ya madaraka, utakatishaji wa fedha, kujihusisha na vitendo vya rushwa, kuongoza genge la uhalifu na kujihusisha na vitendo vya rushwa.

Mbali na Sabaya washtakiwa wengine ni Silvester Nyengu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya(31).

Septemba 9, mwaka huu, kabla ya kuwasomea mashtaka yanayowakabili washatakiwa hao katika mahakama hiyo, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Tersila Gervas, alidai kwamba Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), ametoa hati ya ridhaa ya kuipa mamlaka mahakama hiyo kusikilizwa shauri hilo katika mahakama ya chini badala ya Mahakama Kuu.

"Mheshimiwa Hakimu, DPP ametoa nyaraka mbili za hati ya kuipa ridhaa na mamlaka mahakama ya chini kusikiliza shauri hili la uhujumu uchumi ambalo kwa kawaida lilitakiwa kusikilizwa Mahakama Kuu, hati hizo tumeziwasilisha mahakamani," alidai Tersila.

Awali akisoma mashtaka yanayowakabili washtakiwa hao, mbele ya Hakimu wa Mahakama hiyo, Patricia Kisinda, wakili huyo alidai shtaka la kwanza ni la kuongoza genge la uhalifu kinyume cha sheria ya uhujumu uchumi kifungu cha 57(1) na 60(2) na linawakabili washtakiwa wote.

Ilidaiwa kwamba kwa pamoja washtakiwa hao, Januari 22 mwaka huu, katika maeneo tofauti ya Jiji la Arusha, walifanya vitendo vya uhalifu kwa kujipatia Sh. milioni 90, kwa manufaa yao.

Alidai kwamba shtaka la pili ni la kujihusisha na vitendo vya rushwa na linamkabili mshtakiwa wa kwanza peke yake na ni kinyume cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kifungu cha 15(1B,2) sura ya 329 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019.

Ilidaiwa Januari 22, mwaka huu, eneo la kwa Murombo jijini Arusha, Sabaya alijihusisha na vitendo vya rushwa kwa kumtaka Francis Mroso kumpatia Sh. milioni 90 kwa kumshinikiza ili asitoe taarifa za jinai za mtu huyo za madai ya ukwepaji kodi.

Alidai zaidi kuwa shtaka la tatu ni la kujihusisha na vitendo vya rushwa, linamkabili Sabaya peke yake, kinyume cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Kifungu cha 15(1B,2) sura ya 329 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019.

Kwamba Januari 22, mwaka huu, Sabaya akiwa kwa Mormbo jijini Arusha, alijihusisha na vitendo vya rushwa kwa kujipatia Sh. milioni 90 kutoka kwa Mroso, ili asitoe taarifa za jinai za mtu huyo za madai ya ukwepaji kodi.

Shtaka la nne ni la matumizi mabaya ya madaraka, linamkabili Sabaya peke yake kwamba Januari 22, mwaka huu Sabaya, akiwa katika eneo la kwa Murombo jijini Arusha, alitumia vibaya nafasi yake ya Mkuu wa Wilaya ya Hai, alimtisha Mroso, kumfungulia mashtaka ya kukwepa kodi.

Shtaka la tano ni la utakatishaji wa fedha na linawakabili washtakiwa wote saba, ambapo ilidaiwa Februari 22, mwaka huu, Sabaya kwa kushirikiana na wenzake, wakiwa katika eneo la kwa Murombo jijini Arusha, walijipatia Sh. milioni 90, wakitambua kwamba kufanya hivyo ilikuwa ni zao la vitendo vya rushwa.

TANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001:2015 Certified

# MWITO WA KUTOA MAONI

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni taasisi ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko inayojitegemea, iliyoundwa kwa Sheria ya EWURA Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti kiufundi na kiuchumi sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili. Pia Mamlaka inadhibiti Umeme na Maji Safi na Usafi wa Mazingira kwa kuhakikisha huduma zinazodhibitiwa zinapatikana kwa viwango vya ubora wa kutosha; kwa bei halisi; salama na kwa uhakika; na kwamba watoa huduma wanapata faida halali na stahiki kwenye vitega uchumi vyao.**

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba leseni kujihusisha na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

| S/N | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Leseni |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Asamoil Company Limited, S.L.P 15730, Dar es Salaam. | Eneo la Makumbusho, Wilaya ya Kinondoni Mkoa wa Dar es Salaam. | Azhad Soud (Mtanzania) | Leseni ya jumla ya mafuta |
| 2. | Ngome J&U Group of Companies Limited, S.L.P 194, Dodoma. | Eneo la Msalato, Wilaya ya Dodoma Mjini, Mkoa wa Dodoma. | Zainul Kachwamba (Mtanzania) | Leseni ya jumla ya mafuta |
| 3. | Simba Oil - Kibada Service Station, S.L.P. 40451, Dar es Salaam. | Kiwanja Na 3, Kitalu "J" Eneo la Kibada, Manispaa ya Kigamboni, Mkoa wa Dar es Salaam. | Farid Salim NahDI (Mtanzania) | Leseni ya jumla ya mafuta |
| 4. | Erick Benjamin Mahenge - BEM Filling Station, S.L.P 14, Makete. | Kijiji cha Ruaha Mbuyuni, Wilaya ya Kilolo Mkoa wa Iringa. | Erick Benjamin Mahenge (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 5. | Mabalanga Filling Station, S.L.P 18, Songe-Kilindi, | Kijiji cha Mabalanga, Kata ya Mabalanga, Wilaya ya Kilindi, Mkoa wa Tanga. | Rajabu Salimu Malekela (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 6. | Njombe Filling Station Co. Ltd - Kahama, S. L. P. 411, Njombe. | Kiwanja Na. 227, Kitalu "L", Nyihogo, Wilaya ya Kahama, Mkoa wa Shinyanga. | James M. Mwinuka (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 7. | Fountain Petroleum Ltd, S.L.P. 826, Mtwara. | Kiwanja Na. 446, Kitalu "AA" Eneo la Sokoni, Wilaya ya Mtwara mjini, Mkoa wa Mtwara. | Mehboob Yusuf Osman (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 8. | Alkadi Alphonce Mushumbusi, S.L.P. 99, Kahama. | Kijiji cha Ruti/Buhanga, Kata ya Bwanjai, Wilaya ya Misenyi Mkoani Kagera. | Alkadi Alphonce Mushumbusi(Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 9. | Robert Francis Lowasa, S.L.P. 15883,Arusha. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "D" Eneo la Makuyuni, Wilaya ya Monduli, Mkoa wa Arusha. | Robert Francis Lowasa (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 10. | Costa Investment Company Limited Petrol Station, S.L.P. 111, Mafinga. | Eneo la Kijiji cha Sawala, Wilaya ya Mufindi, Mkoa wa Iringa | Costa Rashid Ng'umbi (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi |
| 11. | Eliasa Shaban Kisisa- Chapakazi Filling Station, S.L.P. 57, Chitego-Kongwa. | Eneo la Chitego, Barabara ya Kiteto, Wilaya ya Kongwa, Mkoa wa Dodoma. | Eliasa Shaban Kisisa (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi |
| 12. | Alutz Co. Ltd, S.L.P 876, Songea. | Kiwanja Na. SS Kitalu "5G", Mtaa wa CCM, Manispaa ya Songea, Mkoa wa Ruvuma. | Hainess William Nanyaro (Mtanzania) | Leseni ya Usambazaji wa Gesi (LPG) |
| 13. | Joseph Augustino, Mdaka, S.L.P 273, Mbinga. | Kiwanja Na. 30, Kitalu "A", Eneo la Masumuni, Mbinga Mjini, Mkoa wa Ruvuma. | Joseph Augustino (Mtanzania) | Leseni ya Usambazaji wa Gesi (LPG) |
| 14. | Kazare Traders, S.L.P. 1166, Musoma. | Kiwanja na. 9, Kitalu "J", Mtaa wa Lumumba, Kata ya Kitaji, Wilaya ya Musoma Mjini, Mkoa wa Mara. | Tuma Kazare (Mtanzania) | Leseni ya Usambazaji wa Gesi (LPG) |

Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote wa leseni hapo juu kwamba asipewe leseni, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**

Jengo la EWURA, Kiwanja Na 3, Kitalu AD, Medeli Magharibi, S.L.P. 2857, Dodoma, Simu: +255 26 2329003-4, Nukushi: +255 26 2329005
Barua Pepe: info@ewura.go.tz • Tovuti: http://www.ewura.go.tz

216461402

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serikali iweke mipango endelevu ununuzi mazao

**KILIO** cha wakulima wa mahindi katika mikoa iliyozalisha kwa wingi ni kikubwa kutokana na kutonunuliwa kwa utaratibu wenye uwazi.

Jambo la kusikitisha na kushangaza ni kwamba serikali inatekeleza kidogo ahadi yake ya ununuzi wa mazao hayo.

Kutokana na hali hiyo, Bunge katika mkutano wa mwezi huu lilitoa maazimio ya kuitaka serikali kuhakikisha mahindi yananunuliwa, huku wabunge wakitaka kuongezwa kwa fedha, ambazo ziliongezwa kuwezesha ununuzi mazao hayo na kuweka kwenye Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB).

Mapema wiki hii, serikali ilitangaza kuanza kununua tani 90,000 baada ya kutoka Sh. bilioni 50, ili kunusuru soko la zao hilo na kila kilo moja ilinunuliwa kwa Sh. 500. Mikoa saba ambayo NFRA itakayoanza kununua ni Ruvuma, Rukwa, Njombe, Songwe, Mbeya, Katavi na Iringa, huku CPB ikinunua mikoa ya Rukwa, Katavi, Njombe, Songwe, Dodoma na Manyara.

Licha ya jitihada hizi, lakini kuna mambo ambayo hayako sawa kwa maana ya kwamba ununuzi wa mazao unafanyika kwa nguvu ya soda, kwa kuwa kama walijipanga vizuri maana yake tungeona tangu awali na yasingetokea malalamiko ya wakulima.

Tunaamini nchi inaongozwa kwa mipango ambayo hupangwa kuanzia ngazi za vijiji na mitaa hadi taifa, na ndiyo maana kuna maofisa kilimo kuanzia ngazi ya chini hadi taifa ambao hukusanya takwimu za wakulima na mazao.

Kutokana na takwimu hizo ni rahisi kujua makadirio ya mavumo kwa zao fulani kwa mwaka huo ni kiasi gani, na namna ya kuhakikisha soko la uhakika kwa wakulima, na kama NFRA itanunua basi wanajua uwezo wao ni kiasi gani kutoka na fedha iliyotengwa na serikali.

Mikoa inayozalisha zaidi inajulikana na kila mwaka inazalisha mazao hayo na mengine, hivyo ni muhimu kukawa na mipango endelevu kuhakikisha yananunuliwa kwa wakati na bei sahihi bila kuwaumiza wakulima.

Tunaona hakukua na sababu ya kusubiri kiongozi wa Chama Cha Mapinduzi aielekeze serikali au Bunge kutoa maazimio na kuitaka serikali kutekeleza, bali kutokana na mipango iliyopo suala hilo lingemalizwa.

Ni muhimu serikali ikahakikisha wakulima wanakuwa na uhakika, na kama kuna kiasi fulani cha bajeti kinatengwa kila mwaka kikafahamika, kutokana na makisio ya mavuno kwa mwaka husika.

Ni matarajio yetu kuwa NFRA itajiendesha kibiashara kama wakala zingine kwa kuhakikisha mahindi ya wakulima yananunuliwa badala ya watu binafsi kununua na kisha kuiuzia serikali.


Malalamiko ya wakulima yamejitokeza Ruvuma, na walieleza wazi kuwa wapo baadhi ya watu serikalini ndiyo wanauza mahindi kwa wakala huku wakulima wakiendelea kusota.

Ni muhimu mipango ikaenda na uhalisia wa mambo kwamba makadirio yanaonyesha mwaka huu kwa sababu mbalimbali, wakulima wanatarajiwa kuvuna kiasi hiki na NFRA inatakiwa kuwa na uwezo wa kununua kiasi fulani na wengine wataruhusiwa kutafuta masoko ya ndani na nje.

Tunashauri kuwa suala hili lisichukuliwe kwa zima moto bali kuwe na mipango endelevu ya ununuzi wa mahindi, kwa kuhakikisha mipango ya kila mwaka ya serikali inaendana na uhalisia.

Haitarajiwi kwa kilichotokea mwaka huu haitarajiwi kijirudie mwakani, ufike wakati kama huu wakulima waanze kuhangaika kupata masoko na wakala ashindwe kununua mazao kama inavyotakiwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Mapitio ya sera yalete nafuu tiba kwa wazee

**KATIKA** kuhakikisha wazee wanapata huduma za afya bila kikwazo, zimekuwa zikifanyika jitihada mbalimbali zikiwamo za kuwapa vitambulisho, ili kuhakikisha kwamba, vinawawezesha kupata huduma hiyo bure.

Hata hivyo, pamoja na jitihada hizo kumekuwapo na malalamiko kutoka kwa wazee kwamba wanakosa huduma hiyo na wakati mwingine kukumbana na lugha chafu kutoka kwa baadhi ya wauguzi.

Ukosefu huo wa dawa na lugha chafu dhidi yao, zinatajwa kuchangia wengine kukata tamaa na wakijihisi wametengwa, hali inayoifanya serikali kuangalia upya Sera ya Taifa ya Wazee, ili iweze kuwa na manufaa zaidi kwa kundi hilo.

Baadhi ya wazee wamekuwa wakidai kwamba, Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003 haina meno kwa kuwa haijatungiwa sheria na kwamba hali hiyo inasababisha wanyanyaswe wanapotaka matibabu.

Kutokana na mtazamo huo, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Dk. Dorothy Gwajima anawahakikishia wazee mambo kadhaa, ikiwamo mapitio ya sera hiyo, ili iwe na manufaa zaidi kwao.

Aliyatamka hayo kuelekea Siku ya Wazee Duniani, ambayo huadhimishwa Oktoba Mosi ya kila mwaka, kwamba serikali iko katika hatua za mwisho za mapitio ya sera hiyo ya mwaka 2003.

Kwa mujibu wa waziri huyo, mapitio hayo yanafanywa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, huku serikali ikiendelea kutekeleza afua mbalimbali zinazolenga kutatua changamoto zinazowakabili wazee.

Mbali na hilo, anasema inaendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuboresha maisha ya wazee, ili kuhakikisha wanapata huduma jumuishi na stahiki, kwa ajili ya ustawi na maendeleo yao.

Anasisitiza kwamba, suala la uboreshaji nafisadi na namna ya kutoa wahudumiaji wazee, ni moja ya vipaumbele vya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na kiongizi wetu, Samia Suluhu Hassan.

Hatua hiyo inayochukuliwa na serikali ni nzuri. Basi ni vyema mapitio ambayo yaendelea kufanywa, yaharakishwe, ili kuondoa malalamiko kwa kundi hilo ambalo linadai kukosa huduma za matibabu inavyotakiwa.

Inawezekana kukawepo asilimia kubwa ya wazee na inawawia vigumu kwenda katika maduka binafsi ya dawa kupata huduma wanazostahili pindi inapojitokeza dawa walizoandikiwa hazipatikani katika hospitali za serikali.

Pendekeza mbadala ni kwamba, kama mapitio ya sera yao kama yatakuja na majibu ya kero za muda mrefu, ambazo wamekuwa na nazo na si vibaya kama watapewa fedha, ili waweze kujigharimia mahitaji yao.

Lakini, wakati serikali ikiendelea kufanya mapitio ya sera, si vibaya kuwadhibiti wauguzi wote wanaowanyanyasa wazee wanaokwenda kupata huduma za afya hospitalini au kwenye vituo vya afya.

Pamoja na hayo, huduma kwa wazee ni dhamana na wajibu wa wote, hivyo na jamii kwa ujumla hawana budi kuwatunza wazee, kwa sababu nguvu zao za uzalishaji mali zimepungua kutokana na kazi waliyoifanya wakiwa vijana.

Wamefanya kazi, kwa ajili ya maendeleo na ustawi wa familia zao na taifa kwa ujumla, wakati serikali ikitimiza jukumu la kuwapa huduma za matibabu bure, jamii nayo ni vyema ikasaidia kuwahudumia, ili kuwapunguzia matatizo.

Kimsingi, kuwahudumia au kuwasaidia wazee ni wa kila mmoja kwa kutambua kwamba wamelitumikia taifa kwa muda mrefu tena kwa namna mbalimbali ikiwamo kuhakikisha vijana wa wanapata mafanikio wanayojivunia sasa.

Ni muhimu kutimiza wajibu wa kuwajali wazee kwa hali na mali ikiwa kama sehemu ya matunda ya uwajibikaji wao kwa taifa, hivyo kila mmoja kwa nafasi yake hana budi kutimiza wajibu wake katika kuhudumia kundi hilo.

# MATANGAZO


Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

## TRAINING INSTITUTE

## KOZI YA WAFANYAKAZI NDANI YA NDEGE (CABIN CREW)

Chuo Cha Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL Training Institute ) kina furaha kuwatangazia watanzania wote kuwa kwa mara nyingine kitaendesha kozi ya wafanyakazi ndani ya ndege (Cabin Crew ) kuanzia tarehe 18/10/2021. Kozi hii ni ya muda wa miezi mitatu (03), chuo kipo uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere-Dar es salaam (JNIA) terminal one kwenye jengo la utawala la ATCL karibu kabisa na kituo cha polisi uwanja wa ndege. Chuo kinakaribisha maombi ya kujiunga na kozi hii kwa wenye sifa zilizoainishwa hapo chini. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 24/09/2021.

**Sifa za mwombaji.**

i. Awe na umri kuanzia miaka 18 hadi miaka 25
ii. Awe timamu kiakili, kimaumbile na urefu kuanzia futi 5"4 na kuendelea
iii. Elimu sio chini kidato cha nne na ufaulu mzuri hasa masomo ya kiingereza, Jiografia na Historia (A,B,C,D)
iv. Aweze kuongea na kuandika kwa ufasaha lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Muombaji mwenye uelewa wa lugha zaidi ya hizi mbili kama Kiarabu, Kichina, Kihindi na Kifaransa atapewa kipaumbele.
v. Awe Mtanzania au raia wa kigeni mwenye vibali halali vinavyomruhusu kukaa au kusoma nchini.
vi. Asiwe na mchoro au tojo ( visible tattoo) kwenye sehemu za mwili zinazoonekana.

**Barua ya maombi iambatane na vitu vifuatavyo.**

i. Nakala za vyeti vya shule/chuo alikosoma
ii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
iii. Picha mbili ndogo (passport size) na picha moja yenye kuonyesha umbo lote ukubwa wa 6x8
iv. Curriculum Vitae –CV
v. Kwa wageni, vibali vya kukaa au kusoma Tanzania

**Fomu ya Maombi ni bure.**
**Maombi yatumwe kwa:**
**Principal**
**ATCL Training Institute**
**Box no 543**
**Dar Es Salaam.**
**Email , training@airtanzania.co.tz**

**Mob: +255735787212 , Landline: +255222842543**
**ATCL TRAINING INSTITUTE.**




**PO Box 123456 / Dar es Salaam, Tanzania**
**Tel: +254 20123456 / Fax +254 20123456 /email:info@airtanzania.com**
**website:www.airtanzania.com**

216462101



# NOTISI / TANGAZO

**AUCTIONEERS AND PROPERTY MANAGERS CO.LTD, CHAMPION AUCTION MART LTD, SUNDI AUCTION MART LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTOR LTD, BEST GROUP LTD, SALEI AUCTION MART,NGOMENI AUCTIONMART LTD, LEGENDS AUCTION MART LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuriya Muungano wa Tanzania, chini ya benki ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa madeni yao pamoja na riba kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 tangu kutolewa kwa tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonesha hapa chini na dhamana zitauzwa kama zilivyo na mahali ziliko.

| JINA LA MTEJA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| FATUMA RASHIDI MASASI | FATUMA RASHIDI MASASI | NYUMBA HATI NO. 87782 | MTAA WA KANUNI – KATA YA MABIBO - UBUNGO | 30/09/2021 SAA 10:00 Kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea |
| HUSSEIN NASIBU JUMA | DEVOTHA FRUMENTUS MBUGA | NYUMBA | MWANALUGALI - KIBAHA | 01/10/2021 SAA 4:00 Kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea |
| JAFARI ATHUMAN JARIBU | AISHA SAIDI KIBAVU | NYUMBA | MTAA WA JUHUDI MBAGALA – TEMEKE | 04/10/2021 SAA 04:00 Kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea |
| ALBERT ROBERT NUMVIRE | ALBERT ROBERT NUMVIRE | Nyumba | KIPAMBA GOGONI | 30/10/2021 Kuanziasaa 4:30 asubuhinakuendelea |
| DANIEL FRANSIS KWAY | DANIEL FRANSIS KWAY | Nyumba | GOBA CHAUREMBO | 03/10/2021 Kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea |
| JOYCE MARIJANI MSOFE | JOYCE MARIJANI MSOFE | Nyumba | KIMARA MICHNGWANI | 02/10/2021 Kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea |
| LETICIA ANDRONIUS KALISA | LETICIA ANDRONIUS KALISA | Nyumba | MALAMBA MAWILI | 05/10/2021 Kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea |
| MILLICENT JESSE BUJIKU | RAMADHANI BARONGO | Nyumba | CHAMANZI MACHIMBO | 03/10/2021 Kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea |
| ALLY SHAWEJI OMARY | ALLY SHAWEJI OMARY | Nyumba | KIPAMBA GOGONI | 02/10/2021 Kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea |
| ALBERT ROBERT NUMVIRE | ALBERT ROBERT NUMVIRE | Nyumba | KIPAMBA GOGONI | 02/10/2021 Kuanziasaa 4:30 asubuhinakuendelea |
| DANIEL FRANSIS KWAY | DANIEL FRANSIS KWAY | Nyumba | GOBA CHAUREMBO | 10/10/2021 Kuanziasaa 4:30 asubuhinakuendelea |
| JOYCE MARIJANI MSOFE | JOYCE MARIJANI MSOFE | Nyumba | KIMARA MICHNGWANI | 05/10/2021 Kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea |
| LETICIA ANDRONIUS KALISA | LETICIA ANDRONIUS KALISA | Nyumba | MALAMBA MAWILI | 05/ 10 /2021 Kuanziasaa 4:30 asubuhinakuendelea |
| MILLICENT JESSE BUJIKU | RAMADHANI BARONGO | Nyumba | CHAMANZI MACHIMBO | 30/09/2021 kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika. Na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada-kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwishailipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. 0754497396
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilicho wekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote

216460502

# Walalamikia tozo ushuru wa huduma

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WAFANYABIASHARA mkoani Mwanza, wamelalamikia tozo ya ushuru wa huduma (Service Levy) wanayokatwa kwenye mapato ghafi kwa kuwa inawaumiza na inachangia kuua mitaji yao na biashara.

Malalamiko hayo waliyaibua jana katika Baraza la Biashara la Mkoa lililofanyika jijini humo na kwamba tozo ya ushuru wa huduma ya asilimia 0.3 inayotolewa kwenye mapato ghafi inaua mitaji yao na kuishauri serikali ushuru huo ukatwe kwenye faida.

Walisema tozo hiyo sio rafiki na ipo haja serikali ikapeleka muswada wa mabadiliko ya sheria, ili tozo hiyo ikatwe kwenye faida badala ya mapato ghafi ili kulinda mitaji yao, vinginevyo uwezo wao wa kuchangia uchumi na mapato ya serikali utapungua.

Mkurugenzi wa JAEGS Ltd, Dk. Elibariki Mmari, alisema kutoza ushuru wa huduma chini ya asilimia 0.3 hakukiuki sheria na kutoa mfano mikoa ya Iringa na Mbeya inatoza asilimia 0.1.

"Suala la tozo ya ushuru wa huduma tumelilalamikia kwenye baraza tangu mwaka 2013 hadi leo, tatizo ni uelewa wa kutafsiri sheria, inaelekeza isiyozidi asilimia 0.3 hata halmashauri zingine zinatoza asilimia 0.2 na nyingine 0.2, hakuna haja ya kupeleka muswada wa mabadiliko ya sheria bungeni," alishauri Dk. Mmari.

Alisema baraza liziagize halmashauri zikae na wafanyabiashara ili kuangalia namna ya kupunguza ushuru huo wa huduma bila kwenda bungeni kubadilisha sheria.

Naye Mwenyekiti wa Wamiliki wa Vituo vya Afya Binafsi, Dk. Felician Ndauzi, alisema matatizo mengine yanahitaji marekebisho ya sheria, lakini pia kuwe na mawasiliano na serikali ili biashara ifanyike vizuri kwa kuwa sasa inafanyika kimtandao. Meneja wa Mamlaka ya Mawasiliano nchini (TCRA), Kanda ya Ziwa, Mhandisi Francis Mihayo, alisema biashara kufanyika kimtandao ni fursa nzuri kwa wafanyabiashara katika kukuza uchumi.

Awali, Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara Wenye Viwanda (TCCIA), Mkoa wa Mwanza, Mwita Kunene, alisema serikali inawacheleweshea wazabuni malipo ya huduma na kusababisha walipe riba kwenye taasisi za fedha. Alisema kuna wafanyabiashara wengi wanakabiliwa na tatizo la upatikanaji wa Mashine za Kielektroniki (EFD's) kutokana na mashine hizo kutolewa na mtu mmoja.

"Kuja kwenye vikao siyo kutuhumiana bali ni muda wa kupata uelewa wa pamoja kuna wafanyabiashara wa wadogo, kati na wakubwa, makundi hayo yote yana kero nyingi ukizingatia zinakinzana na sheria," alissema Kunene.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, aliahidi kutatua shida mbalimbali za wafanyabiashara hao na kuwataka watumishi wa umma kupunguza urasimu na kushawishi rushwa kwa wawekezaji ili wapewe maeneo ya kuwekeza.

Alisema vitendo hivyo vinachangia wawekezaji kushindwa kuwekeza kutokana na urasimu na rushwa ama njoo kesho kunakofanywa na watumishi wa umma wenye dhamana hiyo, ili kufanikiwa kwenye uchumi wa bluu halmashauri zitenge maeneo hayo mapema.

Wafanyabiashara hao wamelalamikia kitendo cha wafanyabiashara wadogo (machinga) kupanga bidhaa na kufanya biashara mbele ya maduka yao.

Walisema hatua hiyo inapunguza mapato ya serikali kwa kuwa wanalipa kodi na ushuru mbalimbali wakati machinga hawalipi chochote.



Mhasibu wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKIC), Mohamed Isimbula (wa pili kulia) akipokea msaada wa fedha taslimu kutoka kwa Kaimu Mkurugenzi Idara ya Fedha Benki ya Exim, Issa Rajabu (kushoto), ikiwa ni mchango wa wafanyakazi wa benki hiyo, ili kusaidia matibabu ya moyo kwa mtoto John Selemani (aliyebebwa na mama yake) kutoka mkoani Tanga, wakati walipomtembelea mtoto huyo katika taasisi hiyo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wahitimu JKT wahimizwa uzalendo

**Na Julieth Mkireri,**

**RUVU**

MKUU wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Meja Jenerali Rajabu Mabele, amewataka vijana wanaohitimu mafunzo ya kijeshi kwa mujibu wa sheria kuzingatia kiapo walichokula na kuwa wazalendo kwa nchi yao. Jenerali Mabele alitoa wito huo juzi, wakati wa kufunga mafunzo kwa mujibu wa sheria. Samia Suluhu katika Kikosi cha Ruvu, Mlandizi wilayani Kibaha, alisema hategemei kusikia vijana waliohitimu mafunzo hayo wanashiriki katika migomo vikuu na badala yake wanatakiwa kuwa wazalendo na kuonyesha nidhamu sehemu yoyote watakayokuwa.

"Tunategemea mtaenda kuwa mabalozi wazuri wa jeshi kwa kuwa wazalendo wa kuilinda nchi yenu. Nitasikitika nikisikia mmeenda kujihusisha na matukio ya uhalifu na migomo vyuoni," alisema.

Mkuu huyo wa JKT pia aliwaeleza wazazi kuwa jeshi hilo halitoi ajira na badala yake linatoa mafunzo kwa vijana wa jeshi la akiba wakiwamo wahitimu wa kidato cha sita. Akifunga mafunzo hayo,

Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Sara Msafiri, aliwataka vijana kutumia vizuri mafunzo ya ujasiriamali waliyopata kujiajiri na kwamba yatawasaidia kuepuka masuala ya ufisadi.

Msafiri alisema ujasiriamali unasaidia kutosheka na mishahara wanayolipwa waajiriwa, hivyo mafunzo hayo yatakuwa dira ya baadaye kwa vijana hao kuyatumia kujikwamua na umaskini, kwenye familia zao kabla na baada ya kupata ajira.

Aidha, aliwasisitiza vijana kutumia vizuri mitandao ya kijamii kujinufaisha na kuchangia maendeleo ya taifa na si vinginevyo.

# Shida upatikanaji majisafi na salama yawatesa

**Na Happy Severine,** MEATU

SHIDA ya upatikanaji wa majisafi na salama kwa wananchi wa mji wa Mhanhuzi, makao makuu ya Wilaya ya Meatu, mkoani Simiyu imeendelea kuwatesa kila mwaka hususani inapofika kipindi cha kiangazi.

Kila mwaka wananchi wa mji huo hukabiliwa upungufu wa maji kwenye bwawa la Mwanyahina ambalo ndicho chanzo kikuu cha huduma hiyo.

Mamlaka ya Maji katika mji huo (Mhanhuzi WSSA), inaeleza kuwa kuwapo maji yenye tope katika kipindi cha kiangazi kunasababishwa na mtambo wa kuchuja maji kuchakaa vifaa vyake ambavyo vimedumu kwa muda wa miaka 12.

Akizungumza jana katika mkutano wa hadhara uliofanyika mjini hapo, Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, alipokea kilio cha wananchi hao wakimwomba awasaidie waondokane na kero hiyo ambayo inawatesa kila mwaka.

Mmoja wa wananchi hao, Bulolelo Daudi, alisema tatizo wanalokabiliana nalo ni pamoja na ukosefu wa maji katika kipindi cha kiangazi. "Mkuu wa Mkoa, tunaomba tukuletee maji ambayo tunayotumia wananchi wako wa mji huu wa Mhanhuzi, sisi hapa shida yetu ni maji, maji, maji...kwani serikali imeshindwa nini kutuletea maji kutoka Ziwa Victoria?" AlihojiDaudi.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Mhanhuzi, Makongo Stephano, alipotakiwa kutoa maelezo kuhusu tatizo hilo, alikiri kuwapo shida hiyo.

"Ni kweli bila ya kuficha, kumung'unya maneno, tunalo tatizo kubwa la maji na tatizo hili limekuwa likitokea kipindi cha kiangazi na mwaka jana hali ilikuwa mbaya zaidi, baada ya chanzo chetu kukauka," alisema Stephano.

Alisema mtambo wa kuchuja maji unazidiwa uwezo na vifaa vyake vimechakaa kutokana na kutumika kwa zaidi ya miaka 12 bila ya kufanyiwa ukarabati upya kama inavyotakiwa.

Stephano alisema mtambo huo ulijengwa mwaka 2009 huku ukilenga kuwahudumia wananchi 24,000 na muda wake ulitakiwa kukoma mwaka 2015 ili ufanyiwe matengenezo upya.

"Licha ya kuzidisha muda wake, watu wameongezeka na kufikia 38,624 hivyo umezidiwa uwezo wake ndiyo maana kipindi hiki huduma inapatikana kidogo kidogo, lakini maji kweli yana tope," alisema Stephano.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa ofisi yake imekuwa ikifanya jitihada za kutatuliwa kwa shida hiyo na kwamba ameshatoa taarifa hadi wizarani, lakini bado hawajapata fedha.

Mkuu wa Mkoa alisema shida hiyo ameipokea na atakwenda kuifanyia kazi huku akiahidi kufanyika jitihada za haraka ili kupata ufumbuzi.

"Juzi tumepokea pampu mbili kutoka wizarani ili kuweza kutatua changamoto hii kwa muda na zitafungwa wiki hii ili ziongeze upatikanaji wa maji, lakini serikali imetupatia Sh. milioni 300 ili kujenga mradi wa maji kutoka Mto Semi ili kuongeza upatikanaji wa huduma," alisema Kafulila.

# Kingu Mjumbe Bodi ya TCCIA

**Na Mwandishi Wetu**

Dk. Said Kingu, daktari bingwa wa magonjwa ya binadamu, amechaguliwa kuwa mmoja wa wajumbe wanane wa Bodi ya Wakurugenzi ya Chemba ya Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA).

Akizungumzia hatua hiyo jana, Mwenyekiti wa Bodi, Paul Koyi, alisifu uamuzi huo na kusema chemba yao kila mara inajitahidi kutumia ujuzi wa wataalamu mbalimbali, ili kuendeleza chemba na jumuiya ya biashara nchini.

"Tunautafsiri uamuzi huu kama hatua nzuri katika maendeleo ya chemba yetu. Kila mara tunajitahidi kutumia wataalamu wetu kuendeleza chemba yetu na kuinufaisha jumuiya ya biashara nchini," amesema Koyi ambaye ni Rais wa TCCIA.

Dk. Kingu aliishukuru jumuiya hiyo kwa kumchagua kuwa mjumbe wa bodi na kusema hiyo ni heshima kubwa kwake. "Nitatumia uwezo wangu na maarifa niliyonayo kutoa mchango stahiki na kuiletea maendeleo chemba yetu na nchi kwa ujumla," aliahidi Dk. Kingu na kuongezea kuwa amejiunga na chemba hiyo kwa sababu ya umuhimu wake katika kujenga uchumi wa nchi.

Alisema siku zote anaamini katika kufanyakazi kwa ushirikiano ndio siri ya mafanikio mahali popote na kuongeza kuwa anaamini kuwa mjumbe wa bod hiyo kutaongeza kasi ya utendaji.

Wajumbe wengine wa bodi ni Njile Bwana, Eutropia James, Judith Karangi ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa TCCIA na Katibu wa bodi, Dk. Meshack Kulwa ambaye ni makamu mwenyekiti (biashara), Swallah Swallah makamu (kilimo), Clement Bocco makamu (viwanda) mwenyekiti Koyi ambaye ni Rais wa Chemba hiyo.

# Shule ya Wazazi CCM yaagizwa ufaulu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Shule ya Sekondari ya Kanawa iliyopo Ukenyenge, wilayani Kishapu mkoani Shinyanga, Donbosco Nyanda, ameagizwa kuongeza kasi ya ufaulu shuleni hapo, ili kutimiza ndoto za wanafunzi.

Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Gilibet Kalima, alibainisha hayo juzi alipofanya ziara ya kikazi mkoani Shinyanga katika shule hiyo ambayo ipo chini ya jumuiya hiyo.

Kalima aliutaka uongozi huo wa shule pamoja na walimu, kubuni mbinu mbalimbali za ufundishaji, ili kuongeza kasi ya ufaulishaji kwa wanafunzi.

Pia alisema mpango wa kufaulisha wanafunzi utasaidia kutimiza ndoto zao pamoja na shule hiyo kuongeza idadi ya wanafunzi kutoka 162 waliopo hivi sasa.

# Magonjwa yanavyoua mifugo wilayani Meatu

**Na Happy Severine,** MEATU

WAFUGAJI wa Wilaya ya Meatu mkoani Simiyu wanaopakana na Pori la Akiba la Maswa na Hifadhi ya Taifa Serengeti wameeleza tatizo kubwa ambalo linatesa mifugo yao hasa ng'ombe kushambuliwa na magonjwa mengi ya ajabu. Wamesema magonjwa hayo yamesababisha ng'ombe wao kufa wengi, huku wakibainisha kuwa unawaathiri zaidi kwa kuvimba mwili mzima, kupasuka kwato, kuvimba mapafu na kutoa udenda.

Walieleza hayo kwa Mkuu wa Mkoa huo, David Kafulila, wakati wa kikao na wafugaji hao.

Walisema magonjwa hayo amesababisha ng'ombe wao wengi kupungua kutokana na kufa, huku wakidai ugonjwa wa kuvimba mwili na kupasuka kwako ndio umekuwa tatizo kubwa. Walieleza kuwa licha ya kuwapo kwa tatizo la malipo, lakini changamoto ya magonjwa hayo ndiyo kubwa zaidi, hivyo wameiomba serikali kuwasaidia upatikanaji wa chanjo ya haraka ili kinusuru mifugo yao.

" Nilikuwa na ng'ombe 80, lakini nimebaki na 37 tu, wengine wote wamekufa kutokana na magonjwa hayo, tunaomba sisi wafugaji hasa tunaopakana na hifadhi serikali itusaidie," alisema Shoka Felesi.

Naye Hunge Hunge, alisema kuwa mbali na magonjwa, changamoto nyingine ni ukosefu wa majosho pamoja na malambo ya kunyweshea mifugo yao.

" Tunayo shida kubwa ya ukosefu wa majosho, ndiyo maana mifugo yetu inapata magonjwa mara kwa mara, lakini hata chanjo hatupati kwa muda mrefu," alisema Hunge.

Ofisa Mifugo wa Halmashauri hiyo, Hussen Nyenye, alikiri kuwapo kwa magonjwa hayo, ambayo alieleza yanasababishwa na mwingiliano uliopo kati ya mifugo na wanyamapori kutoka hifadhini.

" Tatizo ni wafugaji wetu wengi kupeleka mifugo yao kwenye hifadhi, ndiyo maana wanapata magonjwa mbalimbali, lakini tumekuwa tukitoa chanjo ila wanaojitokeza wachache, kwa mwaka huu hatujatoa chanjo," alisema Nyenye.

Kutokana na hali hiyo, Kafulila alimtaka mkurugenzi wa halmashauri kumpatia taarifa ya hadhari inayotokana na magonjwa hayo kujua ukubwa wa tatizo ili kuomba msaada kutoka wizarani.

"Waziri wa Mifugo anatoka Mkoa wa Simiyu, leo nitamweleza tatizo hili ili kuona wanaweza kutusaidia vipi kwa haraka kutatua shida hii, lakini nipate taarifa ya ukubwa wa tatizo hili," alisema Kafulila.

Katika kikao hicho wafugaji waliiomba serikali kuanzisha mkakati wa upandaji wa nyasi za kisasa, ili kukabiliana na changamoto ya malisho pamoja na kupatiwa elimu ya ufagaji wa kisasa.




Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Magharibi, Sospeter Magesse (watatu kushoto), akikabidhi viti mwendo kwa Mkuu wa Wilaya ya Kibondo, Kanali Agrrey Magwaza (katikati), vilivyotolewa na benki hiyo kwa ajili ya Kituo cha Afya Nyaruyoba, wilayani humo mkoani Kigoma, ikiwa ni sehemu ya vifaa mbalimbali vyenye thamani ya Sh. milioni 7. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwinyi apewa kongole ujenzi Bandari Pemba

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WAFANYABIASHARA kisiwani Pemba wamemshukuru Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwa ahadi ya kujengwa bandari ya kisasa Mkoani Pemba, ambayo itasaidia meli za mizigo kufika moja kwa moja.

Hivi karibuni Dk. Mwinyi alikuwa na ziara ya siku nne kisiwani Pemba, ambapo alitembelea miradi mbalimbali na kuzungumza na wananchi na kusikiliza kero zao.

Dk. Mwinyi aliwashukuru wananchi kwa kumchagua kuiongoza Zanzibar, ambapo aliwaahidi kuwatekelezea mambo mbalimbali kuhakikisha nchi inapata maendeleo endelevu.

Wakizungumza na waandishi wa habari hizi kwa nyakati tofauti wafanyabiashara hao walisema wamefarijika sana kusikia kauli ya Rais ya kujenga bandari, kwani wanaamini gharama za bidhaa zitapungua kwa kiasi kikubwa. Walisema bidhaa zinapofika kisiwani Pemba zinakuwa ghali sana, hali ambayo inasababisha wananchi kushindwa kununua na hatimaye kukaa muda mrefu bila kupata wateja.

Walisema ikiwa itajengwa bandari ya kisasa, itasaidia meli za mizigo kuja moja kwa moja kisiwani Pemba, hivyo wanaamini kwamba bei ya bidhaa itashuka na kuwapa wafanyabiashara na wananchi ahuweni.

"Bidhaa tunachukua Dar es Salaam au Unguja, kwa hiyo tunapofika Pemba bei lazima iwe kubwa kwa sababu kila tunapopita tunalipia mzigo na ukiangalia pia tunatakiwa tulipe kodi, hivyo lazima tuongeze bei ili na sisi tujilipe gharama zetu," alisema mmoja wa wafanyabiashara hao.

Mfanyabiashara wa kanga na madera Chakechake, Mbarouk Mohamed Zahor, alisema kauli ya Dk. Mwinyi kutaka kujenga Bandari Mkoani Pemba ni nzuri na anaifagilia sana, kwani anaamini watapata maendeleo kama walivyo wenzao wa nje ya kisiwa hicho.

"Biashara kwa Pemba muda mwingi ni ngumu, lakini hii inasababishwa na kuwa bei ni kubwa na pia mizigo huchelewa kupatikana, hivyo ikiwa itajengwa bandari ya kisasa na mizigo kuja Pemba, itakuwa ni chachu ya maendeleo yetu," alisema..

Mfanyabiasha wa nguo za watoto, Maulid Ali Kassim, alisema wamefarijika sana walipomsikia Rais kuhusu kutaka kuijenga bandari, kwani ushuru utapungua kwa kiasi fulani ukilinganisha na wanapochukua nje ya Pemba.

# TRA sasa kutoa nyaraka za Kiswahili kwa w/biashara

Na Gurian Adolf, SUMBAWANGA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imesema kuwa itaandaa utaratibu ili nyaraka zinazotolewa na mamlaka hiyo kwenda kwa wafanyabiashara ziwe zina andikwa kwa lugha ya Kiswahili ili wawe wanazielewa vizuri.

Mkurugenzi wa Elimu kwa Mlipakodi nchini, Richard Kayombo, alisema hayo jana kwenye kikao kilichofanyika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga, baada ya kupokea ombi kutoka kwa wafanyabiashara wa Mkoa wa Rukwa walioomba nyaraka zinazotolewa na ofisi hiyo kwenda kwao ziwe zinaandikwa kwa lugha ya Kiswahili kwa kuwa lugha ya Kiingereza hawaijui vizuri.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Sadrick Malila maarufu kwa jina la Ikuwo, alisema kuwa wengi wa wafanyabiashara hawana elimu kubwa kwani wao walikimbilia zaidi kutafuta fedha kabla ya elimu ya darasani hivyo lugha ya Kiingereza ni tatizo.

"Wala sio siri, wafanyabiashara wengi hawana elimu kubwa, wengi wetu lugha ya Kiingereza inasumbua kwa kuwa tulichagua kutafuta fedha kwanza kabla ya elimu ya darasani, hivyo tunaomba nyaraka zinazotolewa na TRA kwa ajili ya wafanyabiashara ziwe zinaandikwa kwa lugha ya Kiswahili ili tuwe tunazielewa," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Kampuni ya Kiluswa Civil Engineering and Contracting, Anyosisye Kiluswa, aliiomba TRA kuwa inawafikia walipakodi haraka panafanyika mabadiliko ya sheria za kodi kwa kuwa baadhi ya wafanyabiashara si wafuatuliaji wa mambo mbalimbali ikiwamo mabadiliko ya kisheria kitendo kitakacho ondoa malalamiko kwao.

Kwa upande wake, Kayombo alisema kuwa TRA imepokea ombi lao kuhusu kuandika nyaraka hizo kwa lugha ya Kiswahili na hivi karibuni mchakato huo utaanza na kufikia Desemba, mamlaka hiyo itaanza kutoa nyaraka hizo kwa lugha ya Kiswahili.




Ofisa Mkuu wa Kitengo cha Tigo Pesa, Angelica Pesha (katikati), akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi wa huduma ya mkopo wa muda mfupi ya 'Tigo Nivushe' kwa kushirikiana na Benki ya Absa Tanzania Ltd na kampuni ya JUMO, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto Meneja Mkaazi wa Kampuni ya JUMO, Erick Luyanga na Mkurugenzi wa Kitengo cha Fedha wa benki hiyo, Obeid Laiser. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waandishi wa habari watumaini mapya kwa Waziri Ashatu Kijaji

Na Christina Mwakangale

WAKATI Waziri wa Habari, Teknolojia na Habari, Dk. Ashatu Kijaji, akizungumza na waandishi wa habari kupitia Chama cha Wafanyakazi wa Vyombo vya Habari (JOWUTA), wamemwomba kushughulikia haki zao.

Miongoni mwa haki hizo ni maslahi, ajira na kuondoa sheria kandamizi zinazodidimiza uhuru wa habari.

Mwenyekiti wa JOWUTA, Claud Gwandu, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, akizungumza katika semina kwa waandishi wa habari na wanachama wa chama hicho, akisema upo umuhimu wa wanafani hiyo kupigania haki zao na kuziripoti.

Gwandu alisema kwamba wakati Rais Samia Suluhu Hassan akifanyia marekebisho jina la wizara husika na kuwa Wizara ya Habari na Teknolojia Habari, yapo ambayo yanaisibu taaluma ya habari na kwamba waziri mpya, aanze na hayo.

"Mabadiliko ya wizara yazae mtazamo mpya na sio mabadiliko ya jina pekee, kuondoka michezo kwenye Wizara ya Habari ni sahihi kwa sababu mchezo una vitu vingi na kuifanya tasnia habari kusahaulika. Bado kuna ukandamizaji na uhuru duni wa vyombo vya habari.

"Kosa la kitaaluma liamuliwe kitaaluma kama ilivyo fani ya uhandisi, tabibu. Gazeti linafanyika kosa ambalo limetokana na mtu mmoja mhariri au mwandishi, kwa nini adhabu iwe ya kukifungia chombo au kampuni, inaathiri wafanyakazi wengine," alisema Gwandu.

Alibainisha kuwa hukumu iliyotolewa kuhusu kuondolewa kwa vifungu vinavyokiuka haki Afrika Mashariki, itekelezwe, na kwamba maslahi na ajira kwa wanataaluma hiyo yawe makubaliano ya mkataba ili kuboresha hali za maisha.

Mkurugenzi wa Shirikisho la Waandishi wa Habari na Vyama vya Waandishi (IFJ) Ofisi ya Afrika kutoka Senegal, Pa Louis Thomas, alisema utafiti walioufanya Tanzania ni kati ya nchi zilizo na waandishi wa habari wakujitolea kwa ukanda wa Afrika Mashariki, wakifanya kazi kwenye mazingira duni.

"Inabidi tuwe na umoja kupitia vyama ili kufikisha yanayotusibu. Media ni biashara kubwa duniani, lakini waandishi hasa barani Afrika hawanufaiki. Inafahamika haki ni sawa duniani kote, mfano mwandishi wa kujitegemea nchi zilizoendelea analipwa stahiki zake, bima ya afya na maisha," alisema Thomas.

Mwenyekiti wa MISA-TAN, Salome Kitomari, alisema umoja wa kitaaluma na ushirikiano unahitajika kuzungumzia kuhusu fani hiyo ili kuondoka vikwazo vilivyopo kwenye vyombo vya habari nchini.

"Tuna haja ya kuwa na umoja wa kitaaluma waandishi wa habari ili kuondoka vikwazo kazini. Itakuwa rahisi kupigania maslahi na kuwapo kwa mikataba ya ajira," alisema Salome.

Ziada Kilobo, aliyemwakilisha Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Kajubi Mukajanga, alisema waandishi wa habari wajisemee wao wenyewe matatizo waliyonayo, badala kuegemea upande mmoja zaidi wa kuwasemea wengine.

# Kampuni tatu zazindua huduma 'TIGO NIVUSHE'

Na Mwandishi Wetu

KAMPUNI ya Kidigitali, Tigo Tanzania kwa kushirikiana na Absa Bank Tanzania Limited na JUMO, wamezindua huduma ya mkopo wa muda mfupi ijulikanayo kama 'TIGO NIVUSHE'.

Akizungumza katika uzinduzi huo jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Mkuu wa Tigo Pesa, Angelica Pesha, alisema kuwa kuanzishwa tena kwa huduma hiyo ya TIGO NIVUSHE hasa safari hii kwa kushirikiana na Benki ya Absa pamoja na JUMO inadhihirisha kuwa Tigo Pesa imeendelea kuwa kinara katika utoaji wa huduma za kifedha nchini wakati huohuo, ikiunga mkono jitihada za serikali kupunguza pengo katika utoaji wa huduma za kifedha hasa katika kukopesha sekta ndogondogo.

" Mwaka 2015 tulizindua huduma hii ya TIGO NIVUSHE kwa mara ya kwanza kwa kushirikiana na JUMO, ambapo tuliweza kutoa mikopo kwa wafanyabiashara wadogo wadogo na wakati pamoja na kundi jingine la wale ambao walipata shida kupata mikopo rasmi," alisema Pesha.

Aliongeza kuwa kuanzishwa kwa huduma ya TIGO NIVUSHE wametoa mikopo kwa zaidi ya wateja milioni 2.1 wa Tigo Pesa, na kwamba ushirikiano wao na Benki ya ABSA na JUMO utafungua njia ya kutolewa mikopo zaidi kwa wateja stahiki wa TIGO PESA hasa kuanzia mwezi huu.

"Hii yote ni kutokana na Kampuni ya TIGO kupitia TIGO PESA kuendelea kuwajali na kuwafungulia dunia wateja wake hasa katika utoaji wa huduma za kifedha, wateja waliosajiliwa kikamilifu na watumiaji wa Tigo Pesa mara kwa mara wataweza kukopa kiwango cha kuanzia shilingi 2,000 hadi 1,000,000 kulingana na mahitaji na ustahiki kwa muda wa mkopo wa siku 7 - 30, na wateja wasiostahili wanahimizwa kutumia huduma za Tigo Pesa zaidi kujiongezea uwezo wa kupata mkopo na wanufaika wa TIGO NIVUSHE wanahimizwa kutumia huduma hiyo mara kwa mara na kulipa kwa wakati ili kuongeza kiwango cha kukopa zaidi na zaidi," alisema Pesha.

Alifafanua kuwa ili kupata mkopo wa TIGO NIVUSHE mteja anahitaji kupiga *150*01# , chagua namba 7 huduma za kifedha halafu 4 Tigo Nivushe na ufuate maelekezo, na kwa wale wateja waliothibitishwa kuwa wanastahiki kupata mkopo huu watapiga *150*81# na kufata maelekezo.

ama
ALHAMISI SEPTEMBA 16, 2021
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Simulizi za kukatiliwa watoto na madhara afya zao yalikojificha**



Ukurasa 13

Matumizi ya oksijeni yalivyo shubiri kwa walioko vitandani hospitalini



Ukurasa 14

**Maradhi ya moyo na siri zake zisizojulikana kwa mgonjwa**

# Utamaduni na mfumo wa maisha unavyotosha tiba magonjwa akili

**Na Dk. Raymond Mgeni,**
Mbeya




UGONJWA wa akili ni hali ya hitilafu katika utendaji kazi za akili, pia kufikiri kunakoathiri mtu kukabiliana na hali mbalimbali za kimaisha na mchanganyiko wa jamii.

Mtu anaweza kukabiliana na mabadiliko ya kitabia yanayoweza kuathiri mtu na jamii inayomzunguka kiasi kwamba maneno kama: 'kichaa, 'mwehu' na 'chizi' hutumiwa na jamii, ingawa haistahili kufanya hivyo na ni lugha ya udhalilishaji mkubwa.

Hata hivyo, neno stahili linalopaswa kutumika ni kuwa "mtu kapatwa na changamoto ya akili au ana ugonjwa wa akili."

**CHANZO CHAKE**

Magonjwa ya akili yanasababishwa na athiriko la kazi ya ubongo au vichocheo, kuathiri ubongo, magonjwa ya ndani yasiyopatiwa matibabu haraka, udhaifu wa ubongo wa mtoto utokao na udhaifu tangu kuzaliwa.

Pia, kuna mtu anapojeruhiwa ubongo kupitia ajali au kupigwa, hivyo sababu kubwa ya vinasaba vya urithi wa ugonjwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Matatizo ya akili, pia yanachangiwa na hali ya uhusiano na msongo mkubwa wa mawazo, huku utumiaji vilevi kama dawa, pombe zinazonywewa kupita kiasi zinachangia kuathiri ubongo na hatimaye akili.

Hata hivyo, bado ufahamu wa jamii nyingi kuhusu magonjwa ya akili unaangukia zaidi katika imani vyanzo vya kishirikina na hata ya 'kiroho'.

Hili linatokea pale, ambapo watu wanapokosa kuelewa hali ya mabadiliko inayomtokea mtu akiwa amechanganyikiwa na hilo likavuta, umakini kuwa karogwa au kachezewa.

Mtu anaposikia sauti za visivyoonekana, mahusika 'kuona' ambavyo wengine hawaoni, kuzungumza kusikoeleweka, tabia hasi kama vile, kuvua nguo mbele za watu, jamii inapokea mtazamo wa kushawishiwa na imani mtu huyo ametendwa la kishirikina.

Jamii nyingi husus ani za Kiafrika, imekuwa kawaida si wote wanafuatilia matibabu ya hospitalini au kufahamu ya kisayansi, kukabili kadhia hiyo ya akili. Sehemu kubwa husaka suluhisho kwa mbadala kwenye tiba asili.

Kuna wakati ndugu za wagonjwa ndio washawishi wakubwa wa kutotaka ijulikane kinachomsibu mgonjwa wao wa akili, wakiegemea suluhishi kwenye tiba za jadi. Mara nyingi wanaposhindwa kutibu wagonjwa wao katika tiba za jadi, ndipo wanarejea katika vituo vya afya, tayari wagonjwa wakiwa na hali mbaya, kuliko ilivyokuwa awali.

Ni hatua inayofikiwa, kukiwa tayari ndugu wametumia muda mrefu na gharama kubwa zaidi kutafuta matibabu yasiyo sahihi, huku ikiwa inamuweka mgonjwa katika hatua nzito zaidi za matibabu kuliko kama angewaishwa.

Pia, kuna sura ya kikwazo wagonjwa wa akili wanapata mtazamo hasi kuanzia kwenye ugonjwa wenye hadi visababishi vyake.

Ikumbukwe, wanaopatwa na athari kubwa zaidi ni ndugu, kwani mgonjwa anapofikia utegemezi katika familia na ndugu, anapaswa kumuhudumia kwa kila jambo na wakati mwingine anamuadhibu mgonjwa kwa kumfungia ndani ya nyumba.

Hilio linatokana na jamii, ambayo inawazunguka humchukulia mgonjwa wa akili katika familia kwamba ni mkosi na hata kuifanya familia yao ikatengwa na jamii inayowazunguka.

**SABABU ZA SAYANSI**

Magonjwa yanachangiwa na sababu zinazoelezewa kisayansi, mathalan urithi wa kijamii kutoka kizazi kimoja hadi kingine, magonjwa yanayoathiri ubongo, matumizi ya vilevi, pombe, msongo mawazo kutokana na matukio yenye athari.

Kuna wakati dawa anazohudumiwa mgonjwa, zina asili ya kuathiri mifumo mingine ya mwili kama figo. Mara nyingi, matatizo makubwa ya figo hujitokeza kutokana na matumizi holela ya dawa na hasa za kijadi

Kuna maeneo wanajamii wanapeana tahadhari ya ama kuoa au kutoolewa, kuitenga familia zenye mgonjwa wa akili au kuzuia ushirikiano wa jamii inayowazunguka, wakihofu uwezekano mkubwa wa kuambukizwa maradhi ya akili kutika kwa mwenza wake.

**SIRI YA TIBA**

Si kweli matatizo ya akili yanatibika kijadi, japo dawa zote hutokana na mitishamba na mazao. Matibabu ya hospitalini ndiyo mazuri zaidi, kwani huendana na elimu inayohusu magonjwa ya akili. Mfano wake, mgonjwa anaweza kupatiwa matibabu na hali inapoonekana haijawa tengamavu tabibu, anaweza kufanya marekebisho yenye maboresho katika matumizi ya dawa na haja zingine za kitatibu kumsaidia mgonjwa kupona.

***Mwandishi ni mtaalamu bingwa na anapatikana katika Hospitali ya Rufani Kanda ya Mbeya; Idara ya Afya ya Akili na Magonjwa ya Akili. Mawasiliano yake ni simu: +255 676 559 211 na baruapepe: raymondpoet@yahoo.com***

AFYA

# Simulizi za kukatiliwa watoto na madhara afya zao yalikojificha

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI kupitia Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, inasema ukatili dhidi ya watoto umeshamiri katika maeneo mbalimbali nchini, ikijumuisha ukeketaji, ubakaji na ulawiti.

Mkurugenzi katika wizara hiyo anayehusika na masuala ya Watoto, Sebastian Kitiku, ameiambia Nipashe kuwa takwimu zilizopo, zinaonyesha nchini wanapitia wakati mgumu katika maeneo kama ya ubakaji, ulawiti na ukeketaji.

Anafafanua kwamba kuna tabia ya baadhi ya wanafunzi wanaotoa mimba shuleni na hata mitaani, akirejea mikoa inayoongoza kuwa na idadi kubwa ni: Kigoma, Sumbawanga, Rukwa na Katavi.

Wito wake Kitiku ni kwamba, wazazi na walezi wajenge utamaduni wa kuzungumza na watoto kuwaelewesha na kuepuka maovu ya kijamii na kupunguza ukatili dhidi yao, akitahadharisha kwamba madhara ya simu hadi sasa ni makubwa. Mwaka jana, vitendo vya ukatili vilivyoongoza ni ubakaji jumla yao 5,867 ikilinganishwa na 6,506 za mwaka 2019; na mimba za wanafunzi katika uwiano wa miaka hiyo tajwa, ni 3,631 ikilinganishwa na 2,860.

Kuhusu ulawiti, kulikuwapo matukio ni 1000, ikilinganishwa na 1,405 ya mwaka 2019, wasababishaji wakubwa wakitajwa kuwa ni ndugu wa karibu wa watoto wanaoegemea mazoea.

Wakati sasa kukiwapo mageuzi makubwa ya kutumia teknolojia za habari na mawasiliano, yanayoambatana na vifaa vya elektroniki kama simu na kompyuta.

### WITO KWA WAZAZI

Kitiku anasema kuna makabila wanayokeketa watoto, ikidaiwa ni sehemu ya uvushaji rika. Hata, hivyo inatajwa kuwapo matendo yanayokatazwa na wataalamu kutokana na madhara yake kiafya.

"Mzazi au mlezi anapaswa kutafuta taarifa za uhakika, kabla ya kuridhia mtoto wako kuondoka nyumbani. Ili kuzuia usafirishaji haramu kwa watoto, kutokana na madhara yake," alishauri.

### MADHILA YA UTUMIKISHAJI

Anabainisha kuwatumikisha watoto wenye umri chini ya miaka 15 ni vitendo vya ukatili kwa kurejea Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini mwaka 2004, inawataka waajiri wote iwe wazazi au walezi wasishiriki kuajiri watoto, kwani inakiuka sheria.

Pia, inatajwa ni suala kinyume na kwa mmiliki wa baa, vilabu vya pombe na kumbi za starehe kuruhusu watoto kuingia maeneo usiku, kwani pako kinyume na umri wake, sambamba na marufuku ya mtoto haruhusiwi migodini, kwenye meli na mashamba makubwa.



Wanafunzi wakiwa darasani **PICHA: MTANDAO**

> **"Hayo yote yalikuwa yanatokea mimi nikiwa sijui kutokana na kuwa muda mwingi sishindi nyumbani. Baada ya kuona kuwa afya ya wanangu kila uchwao inazorota, ndipo nilipochukua jukumu la kuwauliza kuwa wanaishije na dada wa kazi.**

Mkurugenzi wa taasisi siyo ya kisrerikali, iitwayo CISEMA yenye vituo vikuu viwili, Tanzania Bara na Zanzibar, haki za watoto, Thelma Dhaje, anasema kazi yao kubwa ni kutetea haki, pia ulinzi na usalama wa mtoto.

Anasema, serikali kupitia Ofisi ya Rais (TAMISEMI) na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, iliweka namba ya simu katika wizara inayohusika na afya, kusaidia kutoa taarifa za ukatili, dhidi ya watoto.

### UKATILI MTANDAONI

Anasema walifuatilia malezi, lishe na makuzi ya awali na wakagundua mtandao wa ukatili na unyanyasaji mtoto, akisisitiza ukati ulio unaongezeka, kinyume na inavyodhaniwa kupungua.

"Huwezi kutofautisha ukatili unaofanyika mtandaoni na unaofanyika katika mazingira ya kawaida. Pia, inawezekana mtoto akafanyiwa ukatili au kubakwa na akarekodiwa katika mazingira ya kawaida na ukahamishiwa katika mtandao, jambo litakalomuathiri maisha yake yote," anasema.

Dhaje anasema duniani watoto wengi ni wapenzi wa katuni za televisheni, simu za mkononi au kompyuta, hivyo wasiokuwa na njema, wanatumia nafasi hiyo kutengeneza programu zinazotambua aliko mtoto na kuangalia katuni kwa intaneti.

Anasema, hilo hufanyika kwa kumtambua aliko mtoto na intaneti hiyo na wanaziweka katika mfumo unaoongea moja kwa moja na mtazamaji, ili kumrubuni.

"Baadae humshawishi avue nguo na kuonyesha maungo yake huku akijirekodi: anasema Dhaje.

### KUTOKA WIZARANI

Anarejea taarifa ya Wizara ya Afya kwamba unyanyaswaji wa watoto kijinsia ikiwamo ukahaba na biashara ya usafirishaji watoto, unawezesha madhara makubwa kimwili, kiakili na kijamii.

Hapo kunaorodheshwa majeraha, ulemavu, ujauzito wa utotoni na vifo kwa wanaojifungua, kudumaa uwezo wa kuelewa, magonjwa ya zinaa na maradhi ya UKIMWI.

Serikali inakiri kwa sasa kuna wasanii wengi wanaounga mkono kupigwaji marufuku ukeketaji na linaadhibika kisheria, ingawaje kuna wasichana wengi wanaosita kutoa taarifa.

### MATUMIZI YA SIMU

Mhadhiri wa Elimu na Saikolojia, kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) Dk. Hezron Onditi, akirejea Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), kwamba zaidi ya watoto milioni 51.2 nchini wanaotumia simu na wanaotumia intaneti wako milioni 28.5, waathirika wengi ni wa simu.

Dk. Onditi, mtafiti wa teknolojia na vyombo vya habari kwa watoto, vijana, ukatili dhidi ya watoto, anasema kuna wazazi wanaowapa watoto wao uhuru uliopitiliza wa kuchezea simu, bila kujua madhara yake.

"Kutumia teknolojia ni haki yao, hatuwezi kuwazuia. Ila kitu tunachokatiwa kufanya ni kuhakikisha kwamba vifaa tunavyowapa wanavitumia kwa usahihi katika kusoma na kujiongezea uelewa na sio kutazama vitu ambavyo vinawaharibu," anashauri.

### WORLD VISION VS MADHEHEBU

Mkurugenzi Msaidizi, Utetezi na Maendeleo ya Watoto, kutoka shirika la World Vision, Dk. Joseph Mitinje, anasema wamejitihidi kutetea haki na maadili yanayomlinda mtoto kiimani na mazingira anayoishi.

Anasema, walishakutana na viongozi wa kidini, kama Baraza la Iddi la Kiislamu na Jumuia ya Kikristo Tanzania (CCT), kutafuta ushirikiano wa kuepusha ndoa za utotoni.Dk. Mitinje anasema alishandaa kitabu kinachomsaidia kiongozi wa kiimani kutoa elimu na kujua namna ya kulinda na kutetea haki za mtoto, pia kudhibiti ukatili dhidi yao.

"Tumefanya hivyo kwa kutembelea madhehebu mbalimbali na kushirikiana nao katika kuelimisha juu ya suala la kulinda haki za watoto kwa kuzingatia mfumo wa kila dhehebu, pia tunashirikiana na wizara ya Afya katika suala mtambuka," anaeleza

Dk. Mitinje anaeleza utafiti umebaini Tanga ndio kinara wa ukatili kwa zaidi ya miaka miwili wa ubakaji, mimba na ndoa za utotoni, ukifuatiwa na Mwanza, Mbeya na Dodoma.

### MFANYAKAZI TISHIO

Rehema Kitururu, mkazi wa Ukonga, Dar es Salaam na mama wa watoto wawili, aliiambia Nipashe namna wanawe walivyopitia madhila ya kuteswa na msichana wa kazi.

Mama huyo mjasiriamali, anayeondoka kila ifikapo asubuhi na kurudi usiku, akiwaacha wanawe na masidi huyo wa nyumbani, anasema kwa kipindi kirefu dada huyo aliwatesa na kuwapa vitisho watoto, iwapo angeeleza wanavyofanyiwa vibaya.

"Hayo yote yalikuwa yanatokea mimi nikiwa sijui kutokana na kuwa muda mwingi sishindi nyumbani. Baada ya kuona kuwa afya ya wanangu kila uchwao inazorota, ndipo nilipochukua jukumu la kuwauliza kuwa wanaishije na dada wa kazi.

"Baada ya kuwauliza walionyesha hali ya hofu. Baada ya kuwabana, walinieleza kwamba hawapewi chakula kwa wakati, siku zingine hawapewi kabisa, wakimuuliza dada wa kazi anawapiga na kuwapa vitisho kuwa watakaposema atawafanya kitu kibaya. Nilipolitambua hilo nilimfukuza nyumbani," anasema Rehema.

Anasema, Baada ya kumfukuza mtumishi huyo, alikuwa anafika nyumbani kwa kuvizia anawatisha watoto huku akiwalaumu kwanini wamesema.

"Nilipoona kuwa anaendelea kuwafuatilia watoto wangu niliendа kumripoti polisi na kumfungulia mashtaka, hivyo nitoe rai kwa wazazi wenzangu kuwa makini na wasichana wa kazi," anaeleza.

AFYA

# Matumizi ya oksijeni yalivyo shubiri kwa walioko vitandani hospitalini

**Na Beatrice Moses**

KUZUKA ugonjwa wa UVIKO -19, ni huzuni, vilio na mateso kwa jamii, ikiwamo kubadili mfumo na mtindo wa maisha kuanzia ngazi familia na duniani kote.

Tanzania nayo ni mdau katika maisha hayo ya kudumu na barakoa, pia kuosha mikono kila mara kwa maji tiririka. Huko nyuma hawakuzoea mambo hayo.

Mchungaji Mstaafu Richard Hananja, ni miongoni mwa waathirika wa UVIKO 19, akisema kuna baadhi ya hospitali zinaiona ni nafasi ya kuvuna fedha kwa kupandisha gharama tiba, penye hitaji la oksijeni.

Hananja, ambaye ni mstaafu wa Kanisa la Kiinjili la Kirutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Mashariki na Pwani, anasema alipougua alipelekwa kwenye hospitali binafsi (jina linahifadhiwa) na alipochunguzwa kitabibu, alibainika kuwa na UVIKO-19.

"Mimi nina bima (ya afya) ya kawaida. Baada ya kufika kwenye hospitali ile, nilijulishwa kwamba bima inalipia kitanda tu, hivyo kuwekewa kwenye gesi napaswa kulipia shilingi milioni mbili taslimu," anasema.

Mchungaji Hananja, anasema lililomshtua mbali na gharama, anaweza kumudu hata kupitia msaada wa waumini asingeshindwa. Lakini, bado anaguswa na swali lenye maumivu; uwezo mdogo wa walio wengi.

### ABUNI MBADALA

Mchungaji Hananja anasema, mtazamo wake hivi sasa ni kujikita zaidi katika maombi, dhidi ya maradhi hayo. Kisa na mkasa? Anafafanua: "Nilikuwa nameza vidonge vingi karibu 20 kwa wakati mmoja kwa siku kulingana na mwongozo wa daktari.

"Nilijikuta shinikizo la moyo likipanda, yaani ukiugua corona kama una kisukari au presha ndiyo inazidi, hivyo unakuwa kwenye hatari ya kupoteza maisha."

Anawashauri viongozi wa dini kuwa makini wanapotoa huduma za kiroho, wasiwe mbali na ushauri wa kiafya katika kupambana na maambukizi ya virusi vya UVIKO-19, pia chanjo zake.

### WANENAYO WADAU

Rehema Ibrahim (siyo jina lake halisi) anaelezea namna familia yao ilivyoangukia pagumu wakati kaka yake alipougua UVIKO-19, akazidiwa hadi kutumia mashine ya kupumua.

"Ni mahangaiko makubwa! Kwanza kufanikiwa kupata huduma hiyo hospitali kadhaa tuliambiwa zimejaa, nikajaribu kutafuta kwenye hospitali nyingine tulipolipata.

"Tukaambiwa kuwa kila mtungi gharama yake ni shilingi laki mbili kwa siku. Aliwekewa mitungi 14, lakini mwisho wa siku alifariki," anasema.

Meneja Uhusiano wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Angela Mziray, anasema tiba gesi, imo katika gharama za bima hiyo, akifafanua:

"Mgonjwa akiwa na bima ina mwongozo wake, lakini kwenye hili la gesi ni tiba, ambayo ipo. Mgonjwa anapobainika anatakiwa kutibiwa kwa kupumulia gesi bima inahusika."

Anashauri mteja anapokabiliwa na hitaji la gesi, awasiliane na NHIF, pia hospitali aliko, ili wafuatilie na kuwezesha kupatikana huduma tajwa.

Dk. Flora Minja, Mwenyekiti wa Baraza la Tiba la Chama cha Kampuni za Bima (ATI), anasema kampuni binafsi za bima zina utaratibu wao wa kuhudumia wateja, kulingana na mwongozo kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima (TIRA).

Anakiri UVIKO-19 umeziweka pagumu kugharamia wanachama wake kibajeti na mwezi uliopita walikutana na kujadiliana magumu yaliyojitokeza kupitia UVIKO-19.

"Tumeona changamoto zake UVIKO-19, tumejadiliana na kila kampuni inashiriki kugharamia tiba hiyo, japo siyo kwa asilimia 10, bali kulingana na bajeti ya daraja la bima aliyokata mteja," anasema Dk. Minja.

### HATUA YA SERIKALI

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, kwenye Mnada wa Msalato, jijini Dodoma mnamo Julai 10 iliyopita, anabainisha watu 284 kati ya 408 walibainika kuwa na UVIKO-19 waliopumua kwa kutegemea mitungi ya gesi tiba.

Mkurugenzi wa Sera na Mipango wa Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Edward Mbanga, anasema serikali inadhamiria kuhakikisha gesi tiba inapatikana kote, ikianzia kanda zote saba nchini.

Ni mtambo unaomudu kuzalisha mitungi 200 ya gesi kwa siku kwenye hospitali zote kubwa za kitaifa, kuhudumia wagonjwa wodini. Mbanga anasema, baada ya kubaini UVIKO -19 imeongeza hitaji la gesi, serikali imeagiza mitambo mingine 12 inayotarajiwa kuwasili karibuni, kutoka nchini Uturuki.

Ni hatua inayochukuliwa huku kukiripotiwa hospitali kuzidiwa wagonjwa wanaohtaji matibabu ya gesi tiba, mfano hai Julai mwaka huu katikia hospitali ya rufani iliyoko Kanda ya Kaskazini.

Mkurugenzi Mtendaji Hospitali hiyo, Profesa Gilleard Masenga, amekaririwa akieleza; kwa siku, kuna wastani inatumika mitungi ya gesi tiba zaidi ya 400, mgonjwa mmoja anatumia wastani wa mitungi minane hadi 10 kwa siku.

Ofisa Habari wa Hospitali ya Rofanui KCMC, Gabriel Chiseo, anasema huduma ya gesi tiba inatolewa kwa gharama ya Sh. 10,000 kwa mtungi, wakiamini ni nafuu na wengi wanaimudu.

"Inapotokea mgonjwa ameshindwa kumudu gharama za gesi tiba, hufanyika utaratibu wa kumsaidia, ili mradi kuhakikisha anatibiwa kulingana na mahitaji ya ugonjwa anaopambana nao," anasema Chiseo.

### UMUHIMU WA GESI

Mtalamu Dk. Ulimboka Ulisubisya, anasema oksijeni ni tiba maalum inayopaswa kutolewa kwa ushauri wa kitaalamu ikifanywa kwa uangalifu mkubwa kwa kuwa mwili kupata nguvu ya oksjeni na inaposewa ni hatari kwa mgonjwa.

"Inahitajika Oksjeni, ili ubongo uwe sawa. Hauwezi kufanya kazi inavyostahili na ikikosekana ndani ya dakika tano au sita ubongo, unakufa hauwezi kufanya kazi. Ndiyo maana inakuwa ya muhimu sana kwa wagonjwa," anasema.

Dk. Ulisubisya anasema wanaougua mapafu, ndiyo wanapata madhara makubwa kwa sababu ni njia ya kuunganishwa na mwili.

"Oksjeni ni muhimu sana, ikikosekana mtu anakufa kwa sababu chembechembe za uhai hazipati hewa kuweza kufaya kazi yake," anasema.

Anafafanua kuwa inahitajika miundombinu itayohakikisha oksijeni ipo wakati wote katika maeneo ya kutoa huduma za afya, kwa kuwa ni dawa muhimu katika kusaidia ahueni ya mgonjwa, hadi kupona.

### HOJA YA WHO

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), kuanzia Januari 3, 2020 mpaka Agosti 31, 2021 kumekuwapo maambukizi 1,367; vifo 50, huku upande wa chanjo hadi Agosti 23 mwaka huu, kuna jumla ya chanjo 218,621 zimeshatolewa kwa wananchi.

Taarifa ya mtandao wa Umoja wa Mataifa zinabainisha kuwa UVIKO -19 imeongeza mara nne mahitaji ya kila siku ya gesi tiba kwa wagonjwa katika nchi za kipato cha chini na kati.

Mkurugenzi wa UNITAID, shirika tanzu la WHO, Philippe Duneton, linawajibikia tiba nafuu duniani, anasema jumla ya watu 500,000 wanahitaji mitungi milioni 1.1 ya gesi tiba kila siku.

Anasema, hadi sasa kuna nchi 25 nyingi za barani Afrika zenye ongezeko la mahitaji ya gesi tiba kutokana na maradhi hayo, yaliyogundulika mara ya kwanza nchini China, Desemba mwaka juzi na hadi sasa inakadiriwa kuua watu 200,000.



Mitungi ya gesi za oksijeni katika hospitali moja kubwa nchini. **PICHA: MTANDAO**

> "Inahitajika Oksjeni, ili ubongo uwe sawa. Hauwezi kufanya kazi inavyostahili na ikikosekana ndani ya dakika tano au sita ubongo, unakufa hauwezi kufanya kazi. Ndiyo maana inakuwa ya muhimu sana kwa wagonjwa.





# Wahudumu wa afya waongoza vituo 95

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa kuna upungufu wa watumishi wa kada ya afya na ustawi wa jamii nchini kwa asilimia 51, huku vituo vya afya 95 vikiongozwa na wahudumu wa afya.

Mwenyekiti wa Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya nchini, ambaye ni Mganga Mkuu wa Mkoa wa Geita, Dk.Japhet Simeo, aliyasema hayo jana kwenye mkutano wao uliofanyika jijini hapa.

"Kuna uhaba mkubwa wa watumishi wa afya na ustawi wa jamii katika vituo vinavyotoa huduma na maeneo mengine ya ustawi wa jamii na watumishi waliopo ni sawa na asilimia 49 na upungufu ni asimilia 51 ya mahitaji ya sasa kulingana na wingi wa vituo na ukubwa wa kazi," alisema.

Hata hivyo, alisema katika uchambuzi wa taarifa zilizowasilishwa kutoka Halmashauri 114 imeonyesha kuwa vituo 95 vinaongozwa na wahudumu wa Afya.

Pia alisema ufinyu wa bajeti katika kulipa stahiki na motisha kwa watumishi ikiwamo fedha ya kujikimu kwa ajira mpya, likizo, uhamisho, matibabu, posho ya masaa ya ziada, posho ya kuitwa mahakamani suala linalosababisha malimbikizo ya madeni kwa muda mrefu na kushusha morali ya watumishi wa Idara ya Afya.

"Vituo kuelemewa na gharama za ulipaji wa mishahara ya wasaidizi wa hesabu kutokana na kukosekana kwa kibali cha ajira na baadhi ya halmashauri kutokuwa tayari kutumia vyanzo vingine vya mapato kulipa mishahara yao," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema kutokuwepo kwa mwongozo wa posho ya madaraka kwa waganga wafawidhi wa vituo vya kutolea huduma za afya ngazi ya msingi.

"Tofauti kubwa ya mshahara na maslahi mengine kwa kada zinazofana lakini zinafanya kazi kwenye taasisi za kutolea huduma za afya zilizo chini ya Wizara ya Afya," alisema.

Aliiomba serikali kuzifanyia kazi kero hizo ili kuboresha mazingira ya kiutendaji katika ngazi ya mamlaka ya mikoa na halmashauri.

# Mikakati 15 kudhibiti wanaosafirisha watoto

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WADAU na taasisi za serikali zinazohusika na kudhibiti tatizo la watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani, wameweka maazimio zaidi ya 15 ikiwamo Jeshi la Polisi kutumia taarifa za kintelejensia kuwakamata mawakala wanaosafirisha watoto na kuimarisha usimamizi wa sheria.

Maazimio hayo yalitolewa juzi jijini hapa kwenye kikao cha kutafuta mwarobaini wa tatizo hilo kilichowashirikisha Makamanda wa Polisi, Makatibu Tawala wa Mikoa, wanazuoni na mashirika yasiyo ya kiserikali. Katika maazimio hayo yaliyotajwa na washiriki hao ni kuwabaini mawakala ambao wanasafirisha watoto kutoka sehemu moja kwenda nyingine na kuwachukulia hatua.

Aidha, kushirikiana kuwatambua watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani na kuwarejesha kwa familia zao, kukagua vyombo vya usafiri na kuimarisha miongozo ya usafirishaji.

Pia azimio jingine ni kuhusisha kamati za ulinzi wa wanawake na watoto, kutambua na kusajili makao ya watoto ili yaendeshwe kwa mujibu wa sheria, kuwa na sheria ndogo za kuwajibisha wazazi ambao wameshindwa kutunza watoto na kutengeneza sheria ya kudhibiti ombaomba kwa kuwa wamekuwa wakiwatumia watoto.

Kadhalika, walishauri ufanyike utafiti kujua idadi ya watoto hao, umri, jinsia na kazi wanazofanya ili kujua ukubwa wa tatizo na kuimarisha utekelezaji wa sheria.

Akifafanua suala la mawakala kwenye kikao hicho, SSP Lucy Ngonyani, anayeshughulikia usafirishaji haramu wa binadamu kutoka Interpol, alisema watoto wengi wanaposafiri kutoka mkoa mmoja kwenda mwingine wanaambatana na mawakala.

"Suala la usafirishaji haramu binadamu Ni suala linalohusisha watu kadhaa, sisi vyombo vya ulinzi na usalama tunaliangalia hilo, tusikimbilie kuhoji watu wazima wao ndo mawakala tukihoji watoto tutajua mambo mengi," alisema.

Akifunga kikao hicho, Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Dk. John Jingu, alisema mawakala wengi wanaotoa huduma za kupata watoto wa kazi za nyumbani hawajasajiliwa.

"Ni jukumu letu sasa kuangalia hawa wanaosaidia watu kupata kazi, wanazunguka mtaani kuchukua watoto hawajitambui na kuwapeleka kufanya kazi kwenye mabaa au nje ya nchi ni kinyume na sheria," alisema Jingu.

Aidha, alisema tatizo la watoto kuishi na kufanya kazi mtaani linatengeneza tatizo kubwa la kijamii, kisiasa kwa kuwa watatumika kuchafua hali ya hewa.

"Tumejadiliana na kuweka maazimio ya jumla na ya kila taasisi ili kutokomeza hali hii, Wizara na taasisi za serikali, polisi, mashirika yasiyo ya kiserikali wote tumetoka na kazi ya kufanya, na tukienda kutekeleza kama tulivyozungumza hili tatizo litakwisha," alisema.

Katibu huyo alisisitiza suala hilo lazima likomeshwe kwa kuwa baadhi ya mikoa haina tatizo hilo.

"Niwaombe twende tukatekeleze haya tuliyokubaliana kwa siku hizi mbili, tuitendee haki nchi yetu ili kuleta ustawi wa maendeleo ya nchi yetu, lakini pia kutoa elimu wengi hawafahamu, kuna siku niliendа kijijini kwetu siku naondoka watu wanataka niondoke na watoto wao, kwenda nao Dar es Salaam nikawaelimisha hakuna kazi ya kuokota angekuwa bazazi angewasomba watoto kupeleka baa na mwisho vinaishia mtaani na kufanya uhalifu," alisema.

Alisema ifanyike kampeni kubwa ya kutoa elimu kwa jamii na kusimamia sheria na miongozo mbalimbali.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akizungumza na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Stergomena Tax, ofisini kwake, Mlimwa, jijini Dodoma, juzi. **PICHA: OWM**

# TAMISEMI yataka usimamizi wa fedha za elimu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imewataka viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wanaoshughulikia sekta ya elimu kusimamia fedha zinazopelekwa kwenye maeneo yao za ujenzi ili kuleta matokeo chanya.

Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Prof. Riziki Shemdoe, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifungua mkutano mkuu wa tatu wa Umoja wa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi Tanzania bara.

Alisema fedha zinazopelekwa kwa ajili ya elimu msingi bila ada na za ujenzi wa miundombinu mbalimbali zinapaswa thamani yake ionekane.

Aliwahimiza kuwa waadilifu na weledi katika utekelezaji wa majukumu yao kwa kufuata miongozo iliyopo.

"Serikali itaendelea kutoa fedha za elimu kwa kuhakikisha inaendelea kujenga miundombinu ya madarasa, nyumba za walimu, vyoo ikiwa ni pamoja na kuweka mazingira mzuri ya kufundishia na kujifunzia," alisema.

Alisema fedha hizo zinapaswa kuleta malengo yanayokusudiwa na kiongozi yeyote atakayeshindwa kusimamia fedha hizo hatua zitachukuliwa.

"Viongozi wenzangu nilisisitize hili la kusimamia fedha ili thamani ya fedha ya kazi tunayopewa tuzifanye ionekane elimu bila ninyi haipo," alisema.

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo anayeshughulikia Elimu, Gerald Mweli, alitoa wito kwa umoja huo kujituma na kuendelea kutekeleza majukumu na kufuata taratibu pale wanapopewa majukumu.

Naye, Mwenyekiti wa Umoja huo, Rehema Ramole, aliishukuru serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa kupandisha madaraja walimu na kuahidi watatekeleza majukumu yao ipasavyo katika kulihudumia taifa kwenye sekta ya elimu.



HABARI MBEYA

# Mabalozi EU watembelea miradi Nyanda za Juu Kusini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MABALOZI wanane wa nchi wanachama wa Umoja wa Ulaya (EU) wanaowakilisha mataifa yao nchini, wameanza ziara maalumu kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo inayofadhiliwa na umoja huo pamoja na nchi wanachama katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Mabalozi hao ni pamoja na Balozi wa EU, Manfredo Fanti, Balozi wa Ubelgiji, Peter Acker, Balozi wa Denmark, Mette Dissing-Spandet, Balozi wa Italia, Marco Lombardi, Balozi wa Uholanzi, Wiebe De Boer na Balozi wa Poland, Krzysztof Buzalski.

Wengine ni Balozi wa Hispania, Francisca Carretero na Balozi wa Sweden, Anders Sjöberg ambao walianza ziara hiyo jana baada ya kufanya kikao na viongozi wa Mkoa wa Mbeya.

Akizungumza kwa niaba ya mabalozi hao, Balozi Fanti alisema moja kati ya miradi wanayokusudia kutembelea ni Mradi wa Uboreshaji wa Mnyororo wa Thamani kwenye kahawa, mhai, mboga na matunda uitwao Agri-Connect.

Alisema katika maeneo yote ya utekelezaji wa mradi huo watakayotembelea, mabalozi hao watakutana na viongozi wa serikali, wabunge pamoja na wakulima wadogo wa mazao hayo ambao ndiyo wanufaika wa kwanza wa mradi huo.

Alisema mradi huo una bajeti ya Euro milioni 103.5 sawa na Sh. bilioni 279 ambazo alisema nusu zinawanufaisha wakulima moja kwa moja na nusu inayobaki ni kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya barabara za vijijini ili kurahisisha usafiri na usafirishaji.

"Mradi huu wa AGRI-CONNECT una lengo la kuleta mabadiliko kwenye sekta ya kilimo kwa kuwasaidia wakulima kuongeza thamani ya mazao yao, kupata masoko ya ndani na nje ya nchi hasa kwenye mazao haya, hivyo mabalozi wote hawa watashuhudia utekelezaji kwenye maeneo yote," alisema Balozi Fanti.

Alisema mabalozi hao waliamua kufanya ziara hiyo ili kujionea kinachofanyika na kuzungumza na wanufaika moja kwa moja ili kujua matatizo yanayowakabili na kwamba mradi huo unawanufaisha wananchi zaidi ya 150,000.

Hata hivyo alisema watatembelea miradi mingine ikiwamo ya afya, sheria, vyama vya waandishi wa habari na miradi mingine ambayo inafadhiliwa na taifa moja moja.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliwapongeza mabalozi hao kwa kuamua kutembelea miradi hiyo na kuwa ziara hiyo itawasaidia kujionea uhalisia wa fedha ambazo mataifa yao yanatoa kwa ajili ya kuwasaidia Watanzania.

Alisema serikali inathamini michango yao na itahakikisha inashirikiana nao katika kila hatua ya utekelezaji ili wananchi wanapate maendeleo kama ambavyo mataifa hayo yanakusudia.

Homera alisema kwa sasa wanaendelea kuhamasisha na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu miradi hiyo ikiwamo ujenzi wa barabara ili waongeze uzalishaji.

"Kwa hapa kwetu Mbeya mradi huu wa Agri-Connect una faida kubwa sana, kuna barabara zinazohudumiwa na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) zinaendelea kuboreshwa kupitia mradi huu na ni fedha nyingi zilizotengwa," alisema Homera.

Kwa upande wake Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, alisema Bunge lipo tayari kuendelea kushirikiana na mabalozi hao kwenye utekelezaji wa miradi hiyo na inalenga kuwasaidia wananchi wa kawaida.



Mbunifu wa mashine ya kuvunia maharagwe na mazao mengine jamii ya mikunde, kutoka Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), Joshua Joasi (wa pili kulia), akitoa ufafanuzi kuhusu utendaji kazi wake kwa Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Aloys Mvuma, wakati wa shughuli za mbio za Mwenge, jijini Mbeya juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wazazi watakiwa kutimiza mahitaji ya watoto shuleni

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Twalibu Lubandamo, amewataka wazazi na walezi wilayani humo kuwa mstari wa mbele, kuhakikisha wanatimiza mahitaji muhimu ya watoto wao wakati wa masomo ikiwamo ununuzi wa sare za shule na uchangiaji wa michango ya shule.

Lubandamo alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na watendaji wa Mamlaka ya Mji mdogo Rujewa, kuwa kauli ya elimu bure imebadilisha mitazamo ya wananchi na kusahau kuhudumia mahitaji ya watoto wao.

Alisema wazazi wengi wamejikita kwenye shughuli za uzalishaji mali na kusahau jukumu la kuwahudumia watoto hao na kuchochea kujiingiza kwenye vitendo visivyofaa kwenye jamii na kuharibu ndoto zao.

"Dhana ya elimu bila malipo imepokelewa vibaya na baadhi ya wazazi kwani hawasikii wala kuelewa jambo lolote linalohusu michango ya shule kama vile madawati, wanamtuma mtoto shule bila daftari wala sare za shule kwa madai kuwa atazikuta huko huko serikali itamnunulia," alisema Lubandamo.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Mbarali, Michael Semindu alisema, mikakati ya wilaya hiyo ni kuhakikisha tatizo la vyumba vya madarasa linashughulikiwa na itakuwa historia kwa kuwa tayari wamekwisha anza kuwahamasisha wananchi kuchangia.

Alisema kwa mwaka wa masomo wa 2021/2022 zaidi ya madarasa 40 yamejengwa katika wilaya hiyo huku hitaji likiwa ni madarasa zaidi ya 100 kwa mwaka wa masomo ujao.

Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji mdogo wa Rujewa, Chameta Godigodi, alisema mamlaka hiyo inakabiliwa na vikwazo mbalimbali ikiwamo kutokamilika kuwa mamlaka kamili na kushindwa kutatua baadhi ya mahitaji.

# Wakulima kufikiwa na teknolojia uvunaji mazao aina ya mikunde

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ZAIDI ya wakulima 800,000 wa zao la maharagwe na mengine ya kunde nchini wanatarajiwa kufikiwa na teknolojia ya uvunaji wa mazao hayo ili kukabiliana na upotevu shambani.

Kwa mujibu wa mbunifu ambaye pia mhitimu wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), Joshua Joasi, alisema teknolojia hiyo ya kisasa itawakomboa wakulima dhidi ya upotevu wa mazao shambani.Joasi alisema mashine hiyo ina uwezo wa kuvuna ekari moja kwa saa moja na ina uwezo wa kuvuna ekari nyingi kulingana na mahitaji ya mkulima.

Alisema mkulima anaweza kuipata mashine hiyo kupitia programu maalum kwenye simu yake ya mkononi inayojulikana kama Lungwana ambayo ndiyo jina la mashine kwa ajili ya kukodi ili akaitumie kwa msaada wa mbunifu.

"Nimevumbua teknolojia hii kwa lengo la kumsaidia mkulima wa maharagwe kunufaika na kilimo chake tumeona mavuno mengi yanapotea shambani kwa sababu ya kutokuwa na teknolojia ya kisasa ya uvunaji, kupitia mpango wa Center of Innovation and Technology tumebuni njia ya kisasa kumsaidia mkulima kuna mazao yake," alisema Joasi.

Aliongeza kuwa mkulima atakodi mashine hiyo ya kuvunia kwa gharama ya Sh. 50,000 kwa ekari moja na akiongeza ekari atalazimika kulipa gharama nyingine.

Baadhi ya wakulima wa zao la maharagwe mkoani hapa wamempongeza kijana huyo kubuni teknolojia ya uvunaji wa zao hilo ambayo itaokoa mazao mengi shambani.

Prisca Mwambepo alisema, kwa sasa anavuna mazao yake kienyeji na asilimia kubwa hupotea na anaamini teknolojia hiyo itakuwa msaada kwao.

Alisema mbunifu huyo ametengeza mashine moja ya kuvunia ambayo imeanza majaribio mkoani Mbeya, lakini mahitaji ni makubwa na amemuomba mbunifu huyo kuongeza mashine nyingine ili kukidhi mahitaji ya wakulima wa maharagwe msimu wa mavuno.



# Zanzibar yakiri uwapo utitiri wa gereji bubu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imekiri kuwapo kwa utitiri wa gereji bubu ambapo watu 282 wametozwa faini na serikali.

Kutozwa kwa faini hiyo kumeingizia serikali Sh. 12,795,500 huku serikali ikichukua juhudi ya kutenga maeneo mengine kwa ajili ya kufanya shughuli hizo.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalumu SMZ, Masoud Ali Mohamed, alisema hayo jana wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Viti Maalumu, Sada Ramadhan Mwenda, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Mwakilishi huyo alihoji juu ya uwapo wa gereji nyingi zilizozagaa na kusababisha uchafuzi wa mji hatua zinazochukuliwa kwa sasa.

Waziri huyo alisema gereji nyingi ziko katika maeneo ya Mji Mkongwe yakiwamo Kokoni, Kidutani na Vikokotoni pamoja na maeneo ya nje ya mji ambayo ni Amani, Mikunguni na Mwanakwerekwe.

Alizitaja juhudi zinazotarajiwa kuchukuliwa ni pamoja na mamlaka ya mazingira kutenga maeneo maalumu ambayo yatatumiwa kwa ajili ya shughuli za matengeneo ya magari.

Waziri huyo alikiri kuwapo kwa gereji bubu ni moja ya athari kubwa za uchafuzi wa mazingira pamoja na mikakati ya serikali ya kuweka usafi wa miji na shehia zake.

"Mwenyekiti wa baraza tayari serikali tumezungumza na wenzetu wa mamlaka ya mazingira ya taifa kwa ajili ya kutenga maeneo maalumu ambayo yatatumika kwa ajili ya matengenezo ya gari," alisema.

# Wataalam wajadili athari corona, mbinu kukwamua uchumi, biashara

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UGONJWA wa Corona umeathiri sekta ambazo zinategemea ushirikiano wa biashara za kimataifa ikiwamo ya utalii ambayo ndiyo sekta mama katika kukuza uchumi wa Zanzibar.

Mwenyekiti wa Kongamano la Watalamu wa Sayansi ya Jamii na Biashara (ICBMEM), Dk Emmanuel Chao, alisema hayo jana mjini hapa wakati wa kongamano la siku tatu hilo lililowashirikisha washiriki kutoka nchi mbalimbali zikiwamo Zambia na Nigeria.

Alisema licha ya corona kuathiri sekta ya utalii, pia imethiri katika maeneo mengine ikiwamo upelekaji wa bidhaa nje ya nchi. Hatua hiyo imesababisha wanunuzi kupungua.

Dk. Chao alisema pia usafiri wa anga umeathirika kutokana na idadi ya wasafiri kutoka taifa moja kwenda lingine umepungua baada ya baadhi ya nchi kuweka vizuizi vya safari.

Kwa mujibu wa Dk. Chao, kongamano hilo limewakutanisha wataalamu wa sayansi ya jamii na biashara kujadili mambo ya uchumi, fedha, utawala, taaluma za kimasomo, ugavi na mambo ya biashara na usimamizi.

Pia alisema mabadiliko ya kiteknolojia na kijamii yameathiri sekta ya biashara, hivyo aliwataka watalamu wa kongamano hilo kujadili mbinu bora za kiutafiti na kuboresha utendaji ili kuwa na mafaniko kwa taifa na dunia.

"Uchumi ni kama mfumo wa mwili, hivyo sehemu moja ikiumwa na zingine zinaumwa. Changamoto nyingi zilizotokea, zimesababisha fedha nyingi ambazo tulikuwa tukizitegemea kupitia fedha za kigeni mianya yake imeathirika," alisema Dk. Chao ambaye pia ni Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu Mzumbe.

Alisema maendeleo pasipo utafiti ni vigumu na utafiti pasipo kuutendea kazi hauwezi kuleta matokeo bora, hivyo aliwasisitiza washiriki wa kongamano hilo kushirikiana ili kuwa na maendeleo bora katika nchi.

Akifungua kongamano hilo, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Simai Muhammed Said, alisema ni jambo muhimu kuunganisha nguvu baina ya sekta binafsi na vyuo vikuu katika kufanya utafiti wa masoko hasa katika kipindi hiki kigumu ambacho dunia inapitia cha janga la corona.

Simai aliwataka washiriki wa kongamano hilo kujadili na kuangalia nchi changa jinsi watakavyoshirikiana katika masoko na ripoti watakazofanya kuziwasilisha serikalini ili kufanyiwa kazi.

"Niwapongeze sana kwa kukutana watalamu wa sayansi ya jamii na biashara hapa Zanzibar. Niseme huu ni mkutano muhimu kwa maendeleo ya nchi na taifa kwa ujumla," alisema.

Naye Dk. Salama Yussuf kutoka Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar, alisema biashara ni masoko na lazima kuwa na wataalamu wa masoko ili kufanya kazi kulingana na viwango bora vya kimataifa, hivyo mada zitakazowasilishwa katika kongamano hilo zitawajengea uwezo watalamu hao jinsi ya kutafuta masoko ya kibiashara.



Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zubeir Ali Maulid (kushoto), akisalimiana na Balozi wa kutangaza utalii ambae pia ni shabiki wa timu ya Taifa Stars, Nicholas Reynolds maarufu kama Bongo Zozo, alipotembelea Baraza hilo, Chukwani jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waathirika wa udhalilishaji waipongeza TAMWA

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAATHIRIKA wa vitendo vya udhalilishaji Zanzibar wamekipongeza Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (TAMWA) Zanzibar kutokana na kuwapatia elimu kufuatilia kesi zao katika vyombo vya kisheria na kuwa tayari kutoa ushahidi mahakamani.

Walitoa pongezi zao juzi mbele ya Naibu Balozi wa Finland mchini Tanzania, Sari Ussi, wakati TAMWA ikiwasilisha ripoti ya utekelezaji wa mradi wa kupambana na matendo ya udhalilishaji Zanzibar Ofisi za TAMWA, Tunguu Zanzibar.

Wahanga hao, ambao watoto wao wamebakwa na kulawitiwa (majina yanahifadhiwa) walisema elimu waliyopatiwa na TAMWA kupitia mradi wa kupamba na vitendo vya udhalilishaji umewajengea ujasiri wa kutoa ushahidi mahakamani ambapo mwenendo wa kesi zao unaendelea vizuri.

Asha Simai (si jina halisi) ambaye mtoto wake mwenye umri wa miaka tisa alibakwa, alisema TAMWA imemsaidia katika kumjengea uwezo na kwenda kutoa ushahidi mahakamani na hatimaye haki imetendeka.

"Naishukuru sana TAMWA imenisaidia mtoto wangu alibakwa na kesi imeshatolewa hukumu. Mshtakiwa kafungwa miaka 30 jela," alisema.

Pia alisema wakati mwingine jamii inaitupia lawama Mahakama kwa kesi za udhalilishaji lakini baadhi ya watu katika jamii nao wana makosa kwa kushindwa kutoa ushirikiano kwa mahakama ikiwemo kutoa ushahidi wakati wanapohitajika.

Alitaka jamii kuachana na muhali kwa kesi za udhalilishaji na kuhakikisha inafuatilia kesi hizo ili haki itendeke na watuhumiwa wachukuliwe hatua za kisheria.

Naye Naibu Balozi Sari alisema amefarijika na matumizi ya rasilimali walizozipatia TAMWA Zanzibar, katika kuongeza kasi dhidi ya mapambano ya udhalilishaji kwa wanawake na watoto.

Balozi huyo alisema ubalozi wa Finland nchini Tanzania unajivunia kufanya kazi na TAMWA katika kipindi chote cha miaka mitatu ya utekelezaji wa mradi huo na umeonesha mabadiliko makubwa kwenye jamii.

Alisema kupitia ripoti hiyo ni faraja kubwa kuona watu wanazungumza mafanikio ya utekelezaji mradi huo ikiwamo watoto wao kutoa ushahidi na hatimaye walihusika kutiwa hatiani.

Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema kabla ya kutekelezwa kwa mradi huo wa kuwajengea uwezo wazee na wahanga wa matukio ya udhalilishaji ilikuwa ngumu baadhi yao kufika mahakamani na kutoa ushahidi.

Alisema kupitia mradi huo, waathirika wa udhalilishaji walijengewa uwezo na hatimaye kutoa ushahidi mbele ya mahakama bila kuwa na chembe ya hofu na kupelekea watendaji wa matukio hayo kuhukumiwa.

Ofisa Utafiti na Tathmini wa TAMWA, Mohamed Khatib, alisema mradi huo wa miaka mitatu kutoka mwaka 2019-2021 ulikusanya makundi mbalimbali yakiwamo ya wazazi wa waathirika, watoto wao pamoja na baadhi ya waandishi wa habari huku lengo likiwa kuwajengea uwezo kuhusu mapambano dhidi ya matendo ya udhalilishaji.

Alisema awali mradi huo ulilenga kuwafikia wanufaika 12,000 lakini walivuka lengo hilo na kuwafikia watu 15,000 katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba.

Alisema jitihada kubwa zilifanyika za kuwajengea wanufaika wa mradi huo uwezo wa kusimama na kutoa ushahidi unaotakiwa sambamba na kufuatilia kesi zao.

"Kwa upande wa waandishi wa habari tuliwajengea uwezo kutambua njia bora za kuripoti na kufanya mwendelezo wa habari wanazozitoa za udhalilishaji," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MATANGAZO MCHANGANYIKO**

PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA ENTEPRISES FINANCE LIMITED (EFL).

KWA MAWASILIANO ZAIDI

**TUPIGIE:0677 111 333**

**AU 0758 112 332**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

---

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA KIGOMA**

**MAHALI KIGOMA**

**MAOMBI NA 221 MWAKA 2021**

**MANENO HILALI......................MWOMBAJI.**
**DHIDI YA**
**TATIZO SHARIF..................MJIBU MAOMBI.**

**WITO KUITWA SHAURINI**
**KWA :TATIZO SHARIF**

Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kutajwa/kusikilizwa **25 Mwezi 1o Mwaka 2021 saa 2.30 Asubuhi** mbele ya Mheshimiwa M . Mwinyi Mwenyekiti wa Baraza la .Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

**AMRI** hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo **tarehe 13 Mwezi 09 Mwaka 2021**

116460302

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya MASWA.**
**Kituo cha ISANGA mkoa wa SIMIYU**
**Usimamizi wa Mirathi Na.02/2021**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YAMAREHEMU MASAMA GUMUSHU WA MWABOMBA-MASWA.**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA LIMI MASAMA.**

**TANGAZO**

*(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)*

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi yamarehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 04 Mwezi Oktoba Mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia:**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuleta mahakamanikukaguliwa.Imetolewa leo tarehe 08 Mwezi 09 Mwaka 2021.

**HAKIMU MKAZI**
**MAHAKAMA YA MWANZO**
**ISANGA.**

116460602

---

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA KIGOMA**
**MAHALI KIGOMA**
**MAOMBI NA 92 MWAKA 2020**
**MWATATU MARIA JUMA HASSAN**
**MWOMBAJI.**
**DHIDI YA**
**TUMAIN AMOS RUSIGWA**
**MJIBU MAOMBI.**
**WITO KUITWA SHAURINI**

**KWA :TUMAIN AMOS RUSIGWA**
**POPOTE PALE ULIPO**

Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kutajwa/kusikilizwa 07 Mwezi 1o Mwaka 2021 saa 2.30 Asubuhi mbele ya Mheshimiwa M . Mwinyi Mwenyekiti wa Baraza la .Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 13 Mwezi 01 Mwaka 2021

116460702

---

## KUPOTEA KWA KADI YA TRACTOR

**EMMANUEL MATHEW MHUNZI**
Anatangaza kwa kupotelewa kwa kadi yake ya **TRECTOR** aina yake **FORD COUNTRY** yenye namba za usajili **T 891 AKS** Kwa yeyote atakae ona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Rb Namba.MOR/MOR/RB/427211/2021**

116460802

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi**
**NO.291/2021**

Ombi la **FURAHA JUMA MKASSY** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **JUMA MUSSA MKASSY**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **tarehe 17/09/2021** kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 14/09/2021**

116460902

---

## KUPOTEA KWA VYETI



**JACQUELINE T. JOACHIM**
Anatangaza kupotelewa na cheti chakuhitimu kidato cha nne index No **S.3747-0017** Shule ya Sekondari Notre Dame na Kidato cha Sita index No **S.0216-0536** Shule ya Sekondari Nganza vilivyotolewa na Baraza la mitihani la Taifa Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa polisi: **DOD/DOD/RB/448042/2021.**

116462002

---

## KUPOTEA KWA KADI YA TRACTOR

PANDA SHOKOLO MAJA ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA TRACTOR YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 606 DJX.** CHASSIS NAMBA **IPY5065EJGP021485.** ENGINE NAMBA **PY3029TZ53168.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/CHU/RB/447540/2021.**

116452502

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **DUNSTAN YOSSE MUDU** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari **TOYOTA NOAH** yenye namba za usajili **T 117 DJK.** Chassis namba **AZR603037802.** Engine namba **1AZ5430429** Kwa yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa Polisi: **DAR/MBU/RB/432543/2021**

116458302

---

**IN THE COURT OF DISTRICT**
**DELEGATE OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE No.78 OF 2021**
**In the matter of the estate of the late**
**THOMAS VICENT LUANDA Of DODOMA**
**And**
**In the matter of an application for letters of Administration by FLORA DANIEL KINAWILO**
**GENERAL CITATION**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filled on or before the 13 day of October 2021
**Dated at Dodoma this 15 day of September 2021.**

116461802

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LUCY YUDA MASWAGA** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 183 DND. CHASSIS NAMBA NZE 1215107861.** ENGINE NAMBA **INZC296859.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/URA/RB/447596/2021.**

116460202

---

## TAARIFA KWA UMMA.



**BW. ADNAN OMARY SHANI**

KAMPUNI YA SALES AND DISTRIBUTION SOLUTION LIMITED, YA S.L.P 33188, MIKOCHENI-DAR ES SALAAM, INAPENDA KUIJULISHA JAMII NZIMA YA WA TANZANIA, KUWA ALIYEKUWA MFANYAKAZI WETU Bw. ADNAN OMARY SHANI, SIYO MFANYAKAZI WETU, KUANZIA TAREHE 27.08.2021, NA TUNAPENDA KUIJULISHA JAMII YA KWAMBA HAUSIKI NA KAZI ZETU ZOZOTE ZILE ZA KIOFISI.

HIVYO BASI KAMA ATAFANYA KAZI AU MAKUBALIANO YOYOTE YALE KWA NIABA YA OFISI BASI KAMPUNI HAITOYATAMBUA WALA HAITOHUSIKA NA CHOCHOTE KILE.

**KWA NIABA YA UTAWALA**

116461002

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No…. Of 2021**

**In the matter of the estate of the late YUDA LOGELI MNYALU Of Nkuhungu within Dodoma**

**And**

**In the matter of application for letters of Administration by STELLA CONRAD MLINGULA**

**GENERAL CITATION**

**(Rule 75 of Probate Rules GN.369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 30 day of 9/2021

**Dated at Dodoma this 8 day of 9/ 2021.**

RESIDENT MAGISTRATE

116461902




TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# TANGAZO


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## MAOMBI YA TAARIFA YA KUONYESHA NIA YA KUTOA HUDUMA YA TEHAMA PAMOJA NA VIFAA VYA TEHAMA KUMBUKUMBU NA. 10007040

TotalEnergies East Africa Midstream B.V. (Kampuni) Tanzania, kampuni ya kimataifa ya nishati, inaalika makampuni/taasisi yenye sifa na uzoefu katika kutoa huduma pamoja na vifaa vya technolojia ya Habari na mawasiliano katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha Mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta hayo katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni karibia kilomita 1,443, kati hizo kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania. Uendelezaji wa Mradi wa EACOP unahusisha uandisi wa kina, ujenzi, uendeshaji na uboreshaji wa miundombinu ya Mradi.

**MAELEZO MAFUPI YA MAWANDA YA HUDUMA:**
Ili kutekeleza majukumu yake, Kampuni inahitaji huduma kutoka kwa wakandarasi wenye uzoefu na sifa nzuri katika kutoa huduma za miundombinu ya mawasiliano pamoja na huduma za mfumo wa kompyuta ikiwemo utatuzi wa changamoto. Huduma zinazotarajiwa ni:

- Utoaji wa huduma za vifaa: kompyuta na mfumo wake, simu na vifaa vinavyoambatana na matumizi ya simu, kufunga mfumo wa umeme na mawasiliano (cabling), mtandao, mfumo wa kuhifadhi taarifa (server) na vifaa vinavyohusiana na huduma hizi.
- Mafunzo kwa timu ya watendaji na watumiaji.
- Huduma za ziada za ushauri (kama vile uundaji, usimamizi wa mfumo, pamoja na ukaguzi).
- Huduma za mawasiliano ya simu.
- Huduma za usaidizi katika uendeshaji pamoja na marekebisho.

**Kama ilivyo katika matakwa ya Kampuni katika vipengele hivi:**
- Kipengele cha kwanza: miundombinu ya mtandao iliyojikita kwenye mfumo wa Cisco.
- Kipengele cha pili: mfumo wa uhifadhi taarifa (server) uliojikita kwenye mifumo ya Microsoft Azure na NetApp.
- Kipengele cha tatu: Mfumo wa kompyuta binafsi uliojikita kwenye mfumo wa Windows, Android na simu za iOS, Microsoft Office 365 na Azure.
- Kipengele cha nne: Mfumo wa usalama mtandaoni.
- Kipengele cha 5: Huduma za kuchapisha.
- Kipengele cha 6: huduma za mawasiliano ya simu.
- Kipengele cha 7: Mfumo wa moja kwa moja (fixed) wa kupata huduma za mtandao.

**VIGEZO MUHIMU:**
Makampuni au taasisi zinazoonyesha nia zinatakiwa kuwasilisha taarifa za:
- Uwezo wa kifedha wa kutekeleza mkataba.
- Uthibitisho wa uzoefu wa kutoa huduma tajwa.
- Uzingatiaji wa Kanuni za Maudhui ya Wazawa za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Wazawa (Nafasi za Ajira na Huduma kwa Watanzania.
- Usajili katika Kanzi Data ya Watoa Huduma wa Ndani ya EWURA (LSSP) katika kipindi cha kuwasilisha nia kwa ombi hili yanahimizwa.
- Mkandarasi LAZIMA awe na cheti cha ushirika cha watendaji/watoa huduma katika soko.

Makampuni yenye nia, uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com (ukubwa usiozidi MB20)** kichwa cha habari kikiwa ni kumbukumbu namba husika hadi kufikia saa **11:00 jioni Majira ya Afrika Mashariki,** tarehe **27 Sept. 2021** Makampuni yaliyokidhi vigezo muhimu pekee ndiyo yatakayopata fursa ya kuwekwa kwenye orodha ya makampuni ya awali yenye vigezo.

216462801

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## OMBI LA TAARIFA YA KUONYESHA NIA (EOI) KWA AJILI YA KUTOA HUDUMA ZA USHAURI WA MAZINGIRA NA UWIMAMIZI NA URATIBU WA TAKA KUMBUKUMBU NA. 10007040

TotalEnergies East Africa Midstream B.V (Kampuni) Tanzania, kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi, inaalika makampuni yenye utaalamu na uzoefu katika kutoa Huduma za Ushauri wa Kimazingira na kushauri kuhusu Usimamizi na Uratibu wa Taka, kutuma nia ya kutoa huduma katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA MAWANDA YA HUDUMA:**
Kampuni inahitaji huduma kutoka kwa makampuni yaliyobobea katika kutoa huduma za Ushauri wa Mazingira na kushauri kuhusu kipengere maalumu cha Usimamizi na Uratibu wa Taka na kitahusisha:
- Utambuzi wa namna ya kuepuka na kupunguza uzalishaji wa taka katika maeneo ya kazi hatakabla ya kufikiria usimamizi wa taka hizo nje ya Mradi.
- Utambuzi na ukaguzi wa wakandarasi wa wa taka kuanzia katika ngazi ya eneo husika, wilaya, mkoa na taifa, kutathmini miundo mbinu ya taka na fursa zinazofaa ili kukidhi mahitaji ya ujenzi wa Mradi.
- Kufanya ukaguzi wa Usalama wa Afya na Mazingira kwa wakandarasi wa kusimamia uchafu pamoja na miundombinu ya uchafu.
- Ubainishaji wa kina wa usimamizi wa taka uliojikita katika makadirio ya taka zitakazozalishwa na Mradi pamoja na suluhisho la mwisho la usimamizi wa taka hizo.
- Uboreshaji (Marudio) wa Mkakati wa Usimamizi wa Taka.

**VIGEZO MUHIMU:**
Makampuni au mashirika yatakayoonesha nia, yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:
- Uzoefu, utendaji, na uwezo katika kutoa huduma za ushauri wa masuala ya mazingira na hasa majukumu yaliyotajwa hapo juu katika usimamizi wa taka katika Miradi Mikubwa nchini Tanzania, na kwa kuzingatia viwango vya kitaifa na Kimataifa ikiwemo viwango vya Shirika la Kimataifa la Fedha (IFC). Kampuni iwe na uzoefu/utendaji usio wa chini ya miaka 5 kwa hapa nchini Tanzania au hata Kimataifa, katika kutoa huduma zote zilizoainishwa.
- Kuwa na wafanyakazi viongozi na wenye kukidhi vigezo na wazoefu katika ukaguzi wa masuala ya Afya, Usalama na Mazangira katika miundombinu ya kusimamia taka katika miradi ya mafuta na gesi inayozingatia vigezo vya kimataifa vya Shirika la Fedha (IFC).
- Uwezo wa kifedha kuweza kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha mahesabu ya fedha ya mwaka 2020.
- Usajili katika Kanzi Data ya Watoa Huduma Wazawa ya EWURA (LSSP) katika kipindi cha kuwasilisha nia kwa ombi hili yanahimizwa.
- Uthibitisho wa sera ya kampuni ya Ubora, Afya, Usalama Kazini na Mazingira (QHSE), taratibu na mchakato unaozingatia viwango vya nchi husika na viwango vya kisekta/kiutaalamu katika kazi kama hizi.
- Usajili na leseni stahiki kutoka kwenye mamlaka za hapa nchini kwa ajili ya kutoa huduma hizo.
  - Uthibitisho wa usajili katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na Cheti cha Mwaka wa Karibuni cha Malipo ya Kodi.

Makampuni yenye nia, uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com (ukubwa usiozidi MB20)** kichwa cha habari kikiwa ni kumbukumbu namba husika hadi kufikia saa **11:00 jioni Majira ya Afrika Mashariki,** tarehe **21 Septemba 2021.**

**Muhimu: Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA).**

216462701

MECHI KALI
HOME
LEICESTER
2.29 | 3.45 | 3.00
NAPOLI
AWAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 499
1 WEKA PESA.
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4 - WEKA PESA.
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
SEND
vodacom m-pesa airtel money tigo pesa EZYPESA halopesa
2 WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# TUCHEL: HUYU LUKAKU ANATISHA DIMBANI



**LONDON,** England

BAO la ushindi la Romelu Lukaku limeonyesha kwa nini Chelsea walimsajili yeye, kwa mujibu wa kocha Thomas Tuchel baada ya kikosi chake kupata ushindi wa 1-0 dhidi ya Zenit kwenye mchezo wa ufunguzi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Lukaku hilo lilikuwa bao lake la kwanza kwa 'Blues' hao kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, juzi Jumanne.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji sasa ana mabao manne kwenye mechi tatu dhidi ya klabu za Urusi na ni Robert Lewandowski, Erling Haaland na Bruno Fernandes tu ndio wamefunga zaidi kuliko Lukaku, mabao 14 kwenye mashindano ya Mabingwa Ulaya tangu msimu wa 2019-20 aliposajiliwa Inter.


Tuchel alimsifia mshambuliaji huyo wa zamani wa Manchester United ambaye alitua Chelsea kwa ada iliyoweka rekodi.

Na Tuchel amesema kiwango chake bora kimethibitisha kwa nini waliamua kumsajili.

"Kilikuwa kichwa bora kabisa (kutoka kwa Lukaku kwa lile bao), akiunganisha vizuri krosi ya (Cesar) Azpilicueta," alisema Tuchel akiiambia BT Sport baada ya mchezo huo.

"Alikuwa hodari kutosha kuweza kuwazidi wengine na kupiga mpira kwa kichwa. Hiyo ndio sababu kwa nini yeye (Lukaku) yupo hapa.

"Anapenda kufunga tena kwenye mechi muhimu zaidi kwetu na hakika amethibitisha ubora wake kwetu."



## *Kane ajipanga kuongeza mkataba*

**LONDON,** England

NYOTA wa Tottenham Hotspur, Harry Kane yupo tayari kuongeza mkataba wake kama utawekwa kifungu cha kumruhusu kuondoka, kwa mujibu wa Eurosport.

Kane alijaribu kutaka kuondoka Tottenham, lakini mambo hayakwenda kama yalivyopangwa kabla ya kufungwa kwa dirisha la uhamisho kwa kipindi cha majira ya joto.

Licha ya nia ya kutoka kwa Manchester City, Kane amebakia hapo kwenye Jiji la London na Spurs.

Kane aliweka wazi mapema msimu uliopita kwamba, anataka kwenda kutafuta changamoto nyingine, lakini Spurs hao hawakuwa tayari kumwachia.

Lakini sasa kwa mujibu wa ripoti hiyo, Kane atakubali tu ofa ya mkataba mpya kama atawekewa kipengele cha kuondoka atakapowaniwa na klabu nyingine.

Nahodha huyo wa England mkataba wake wa sasa umebaki miaka mitatu na Spurs wanataka kumwongeza.

Paris Saint-Germain, Juventus, Real Madrid na Barcelona awali nazo zilikuwa zinahusishwa na Kane.

## HABARI MICHEZO

,059,740

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

**BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13**

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 18.9.21 | 17:00 | Derby vs Stoke City | 3.00 | 3.15 | 2.36 |
| 2. 18.9.21 | 17:00 | Millwall vs Coventry | 2.47 | 3.17 | 2.82 |
| 3. 18.9.21 | 17:00 | Cardiff vs Bournemouth | 2.86 | 3.31 | 2.36 |
| 4. 18.9.21 | 17:00 | Barnsley vs Blackburn | 2.77 | 3.16 | 2.52 |
| 5. 18.9.21 | 18:00 | Lens vs Lille | 2.49 | 3.29 | 2.79 |
| 6. 18.9.21 | 19:30 | Aston Villa vs Everton | 2.46 | 3.27 | 2.92 |
| 7. 18.9.21 | 19:30 | Elche vs Levante | 2.67 | 3.13 | 2.77 |
| 8. 18.9.21 | 22:00 | Alaves vs Osasuna | 3.02 | 3.12 | 2.48 |
| 9. 19.9.21 | 13:30 | Empoli vs Sampdoria | 2.52 | 3.63 | 2.62 |
| 10.19.9.21 | 14:00 | Nice vs Monaco | 2.73 | 3.38 | 2.48 |
| 11. 19.9.21 | 16:00 | Brighton vs Leicester | 2.83 | 3.19 | 2.58 |
| 12. 19.9.21 | 17:15 | Real Sociedad vs Sevilla | 2.56 | 3.17 | 2.86 |
| 13. 19.9.21 | 21:45 | Juventus vs AC Milan | 2.36 | 3.32 | 3.03 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

**ALHAMISI - 16 - SEPTEMBA 2021**

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 17:00 | 1628 | Lokomotiv Tashkent vs Surkhon Termez | 1.42 | 4.16 | 6.58 |
| 17:00 | 1637 | Concordia Chiajna vs Unirea Slobozia | 1.93 | 3.19 | 3.77 |
| 17:00 | 4111 | Sogdiyona Jizzax vs Bunyodkor | 2.76 | 3.14 | 2.42 |
| 17:00 | 5087 | Keciorengucu vs Boluspor | 1.77 | 3.53 | 4.06 |
| 17:00 | 5126 | Nasaf Qarshi vs Qizilqum | 1.51 | 3.88 | 5.63 |
| 17:00 | 5689 | NK Aluminij vs Luka Koper | 4.10 | 3.40 | 1.92 |
| 17:30 | 4448 | Kairat Almaty vs Omonia Nicosia | 2.25 | 3.20 | 2.96 |
| 18:00 | 2776 | Al-Shamal vs Al-Sailiya SC | 3.49 | 3.39 | 1.95 |
| 18:30 | 1083 | Magallanes vs Puerto Montt | 2.26 | 3.04 | 3.09 |
| 18:30 | 1755 | Al Ahli Manama vs Manama Club | 3.06 | 3.01 | 2.29 |
| 18:35 | 4508 | AL Baten vs AL Tai | 1.68 | 3.98 | 4.47 |
| 19:00 | 2698 | GKS Katowice vs Arka Gdynia | 3.15 | 3.30 | 2.11 |
| 19:00 | 5766 | JBK Pietarsaari vs Narpes Kraft | 1.79 | 4.07 | 3.44 |
| 19:45 | 1148 | Rapid Vienna vs Racing Genk | 2.51 | 3.51 | 2.66 |
| 19:45 | 2066 | Bayer Leverkusen vs Ferencvaros TC | 1.23 | 6.19 | 11.97 |
| 19:45 | 2379 | Karabakh vs FC Basel | 3.19 | 3.33 | 2.08 |
| 19:45 | 2831 | Lincoln FC vs PAOK | 13.26 | 5.69 | 1.19 |
| 19:45 | 2900 | Midtjylland vs Ludogorets Razgrad | 1.80 | 3.69 | 4.29 |
| 19:45 | 3204 | Flora Tallinn vs KAA Gent | 6.58 | 4.45 | 1.39 |
| 19:45 | 3495 | Slavia Prague vs Union Berlin | 2.51 | 3.34 | 2.51 |
| 19:45 | 3570 | Red Star Belgrade vs Sporting Braga | 2.20 | 3.49 | 3.14 |
| 19:45 | 3818 | Slovan Bratislava vs Copenhagen | 4.26 | 3.40 | 1.77 |
| 19:45 | 4514 | Galatasaray vs Lazio | 3.55 | 3.75 | 1.95 |
| 19:45 | 4530 | Dinamo Zagreb vs West Ham | 3.15 | 3.55 | 2.17 |
| 19:45 | 4864 | Lokomotiv Moscow vs Marseille | 3.30 | 3.70 | 2.06 |
| 19:45 | 4874 | Rennes vs Tottenham | 2.71 | 3.20 | 2.42 |
| 19:45 | 5408 | HJK Helsinki vs LASK Linz | 2.48 | 3.30 | 2.57 |
| 19:45 | 5516 | NK Mura vs Vitesse Arnhem | 4.54 | 3.86 | 1.62 |
| 19:45 | 5764 | Betis vs Celtic | 1.68 | 3.95 | 4.71 |
| 20:00 | 1222 | IFK Varnamo vs Jonkopings Sodra | 2.01 | 3.41 | 3.71 |
| 20:00 | 2146 | Istanbulspor vs Ankaragucu | 2.05 | 3.20 | 3.39 |
| 20:00 | 4822 | Cobreloa vs Union San Felipe | 2.38 | 3.01 | 2.92 |
| 20:15 | 2605 | Qatar SC vs Al Sadd SC | 6.58 | 5.03 | 1.34 |
| 20:15 | 5498 | Al Arabi Doha SC vs Lekhwiya SC | 4.75 | 3.97 | 1.58 |
| 20:30 | 4759 | AL Salt vs Wihdat Amman | 3.43 | 3.19 | 2.04 |
| 21:00 | 2872 | Al Hidd Club vs Najma Manama | 1.81 | 3.58 | 3.82 |
| 22:00 | 1248 | Leicester vs Napoli | 2.29 | 3.45 | 3.00 |
| 22:00 | 2094 | Brondby vs Sparta Prague | 2.69 | 3.39 | 2.54 |
| 22:00 | 2133 | Anorthosis Famagusta vs Partizan | 3.28 | 3.09 | 2.14 |
| 22:00 | 2172 | Rangers vs Lyon | 2.61 | 3.51 | 2.56 |
| 22:00 | 2322 | Eintracht Frankfurt vs Fenerbahce | 1.69 | 4.00 | 4.60 |
| 22:00 | 3119 | Roma vs CSKA Sofia | 1.18 | 5.80 | 13.52 |
| 22:00 | 4289 | Baumit Jablonec vs CFR Cluj | 2.86 | 3.05 | 2.39 |
| 22:00 | 4413 | PSV Eindhoven vs Real Sociedad | 2.33 | 3.56 | 2.86 |
| 22:00 | 4852 | Monaco vs Sturm Graz | 1.42 | 4.70 | 7.00 |
| 22:00 | 4911 | Randers vs AZ Alkmaar | 3.53 | 3.39 | 1.94 |
| 22:00 | 5165 | Olympiakos vs Royal Antwerp | 1.67 | 4.01 | 4.71 |
| 22:00 | 5246 | Bodo Glimt vs Zorya Lugansk | 1.70 | 3.58 | 4.36 |
| 22:00 | 5795 | Juventud LP vs Villa Teresa | 1.34 | 4.46 | 8.14 |
| 22:15 | 4498 | Academica vs CF Estrela | 1.92 | 3.32 | 3.81 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



# DYBALA ATARAJIA MKATABA MPYA

**TURIN,** Italia

PAULO Dybala ameelezea mpango wake wa kumaliza sakata la kutia saini mkataba mpya na Juventus baada ya kuwasaidia miamba hao wa Serie A, kupata ushindi, dhidi ya Malmo kwenye mchezo wa ufunguzi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Dybala alifunga bao la pili la Juve kwa mkwaju wa penalty, Jumanne wakati wakipata ushindi wa 3-0, dhidi ya miamba ya hao wa soka la Sweden.

Hata hivyo, Dybala amebakiwa na mwaka mmoja tu kwenye mkataba wake wa sasa na nyota huyo mwenye umri wa miaka 27, anaweza kuondoka kwa uhamisho huru mwishoni mwa msimu huu.

Makamu Rais wa Juve, Pavel Nedved, hivi karibuni alibainisha kwamba, nyota huyo wa zamani wa Palermo yupo katikati ya mradi wao na ana uhakika wanaweza kufikia makubaliano.

"Kuhusu mkataba mpya? Mara zote najaribu kuwa kwenye ubora," alisema Dybala akiiambia Sport Mediaset baada ya mchezo huo.




shindi wa bonasi ya Jackpot, Juma Idd Mollel, kutoka rusha akionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 32.2 aada ya kushinda bonasi ya Jackpot kutoka Sport-esa. Juma alibashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 Jackpot kwa kuweka kombinesheni za mechi tano keka mmoja. Jackpot ya SportPesa kwa sasa imefikia h. 499,059,740. PICHA: SPORTPESA

# *Lewandowski achekelea kuitungua Barcelona*

**BARCELONA,** Hispania

ROBERT Lewandowski ameelezea ushindi wa Bayern Munich pale Camp Nou kama "siku njema" baada ya kufunga mara mbili katika ushindi wa 3-0, kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, dhidi ya Barcelona.

Bayern ilianza vizuri msimu mpya wa 2021-22, kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa ushindi mnono pale Barca, juzi Jumanne, huku Thomas Muller akifunga bao la ufunguzi.

Lewandowski amefunga katika mechi 18 zilizopita za Bayern, akitikisa nyavu mabao 29.

Katika misimu mitatu iliyopita tangu mwanzoni mwa msimu wa 2019-20, Lewandowski amefunga mabao 113, kwenye mechi 93 kwa Bayern - 36 zaidi ya mchezaji yeyote Ulaya katika ligi kubwa tano kwa muda huo (Kylian Mbappe na Cristiano Ronaldo wana mabao 76 kila mmoja).

"Mara zote ni vizuri kuwa uwanjani kusikia wimbo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya mbele ya watazamaji. Hakika ni hisia nzuri sana," alisema Lewandowski akiwaambia waandishi wa habari mara baada ya mchezo huo.

"Kwa uhakika, uwanja haukujaa, lakini kila kitu kitarudi kama kawaida hivi karibuni."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO ALALAMA MAN UNITED KUPOTEZA UEFA

●●● Hayakuwa matokeo tuliyoyataka, lakini ni muda wa kujipanga na kuangalia mchezo unaofuata...

**MANCHESTER,** England

CRISTIANO Ronaldo amelalamika Manchester United kupoteza dakika za majeruhi dhidi ya Young Boys kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini nyota huyo anaangalia uwezekano wa kuamka haraka kwa 'Mashetani Wekundu' hao.

Ronaldo alifunga bao lake la tatu katika mechi mbili alizoichezea United tangu arudi, lakini vijana hao wa kocha, Ole Gunnar Solskjaer walijikuta wakipoteza kwa mabao 2-1 baada ya Jordan Siebatcheu kuiwahi pasi ya Jesse Lingard na kufunga dakika ya 95.

**Akiwa amefikia rekodi ya mchezaji mwenzake wa zamani wa Real Madrid, Iker Casillas ya kucheza mechi 177 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya juzi Jumanne, Ronaldo alifunga bao la uongozi dakika ya 13 kwenye mchezo huo wa ufunguzi wa Kundi F.**

United kwenye mchezo huo walimaliza wakiwa na wachezaji 10 baada ya beki wa pembeni, Aaron Wan-Bissaka kutolewa nje dakika 10 kabla ya mapumziko.

Ronaldo, ambaye atasafiri na United kwenda kucheza na West Ham Jumapili kweye Ligi Kuu, aliandika kwenye kurasa wake mtandao ya kijamii akisema: "Hayakuwa matokeo tuliyoyataka, lakini ni muda wa kujipanga na kuangalia mchezo unaofuata!"

"Ni wakati wa kusahau na kujikita zaidi kwa ajili ya mchezo unaofuta, naamini mambo tayakuwa sawa tu."

Mchezaji huyo, 36, alirudi hapo United baada ya kuondoka miaka 12 na siku 132 zilizopita.

## ZISIKUPITE

### KANE NA MKATABA SPURS

MSHAMBULIAJI wa England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 28, huenda akatia saini mkataba mpya na Tottenham Hotspur iwapo kifungu cha kumwachia kuondoka katika mkataba wake kitawekwa. Nyota huyo awali aliamini kwamba alikuwa na makubaliano ya kiungwana na Mwenyekiti wa klabu hiyo, Daniel Levy, kuondoka Spurs msimu huu wakati Manchester City ilipojaribu kumsajili. ***(Eurosport)***

### TIELEMANS NA HATIMA YAKE

KIUNGO wa kati wa Ubelgiji, Youri Tielemans, amesema anaweka hatima yake wazi huku akiendelea kujadiliana kuhusu mkataba wake na klabu ya Leicester. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, amehusishwa na uhamisho wa Liverpool, Manchester United, Barcelona na Real Madrid. ***(Sky Sports)***

### MARTINEZ KAGOMBEWA ULAYA

TOTTENHAM Hotspur na Atletico Madrid zote ziliwasilisha ombi la dau la euro milioni 90 kumsajili mshambuliaji wa Argentina, Lautaro Martinez, ambalo lilikataliwa na klabu ya Inter Milan msimu huu, huku Arsenal pia ikakataliwa baada ya kutoa ofa ya chini. ***(Gazzetta dello Sport)***

### SAKA AZIDI KUWA LULU

MSHAMBULIAJI wa Arsenal na England, Bukayo Saka amefuatiliwa na klabu tofauti, lakini 'Washikabunduki' hao wamekataa kumwachia. ***(Here We Go podcast, via Sun)***

### WIRTZ ATAKIWA EPL, BAYERN

KIUNGO wa Bayer Leverkusen mwenye umri wa miaka 18, Florian Wirtz amevutia nia kutoka kwa baadhi ya klabu za Ligi ya England (EPL), na Bayern Munich. ***(Express)***

### KOUNDE BADO HAKIELEWEKI

FURSA ya Chelsea ya kumsajili beki wa kati wa Sevilla mwenye umri wa miaka 22, Jules Kounde itategemea iwapo mkataba wa beki wa Ujerumani, Antonio Rudiger na mabingwa hao wa Ulaya utatatuliwa. ***(Star)***

### ARSENAL WAKOMAA NA AOUAR

ARSENAL haijafutilia mbali matumaini ya kumsajili kiungo wa kati wa Lyon na Ufaransa, Houssem Aouar na itamlenga mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 msimu ujao. ***(Todofichajes)***

### NANDEZ AWA LULU ULAYA

KLABU ya Tottenham Hotspur inatarajiwa kuwa miongoni mwa klabu zitakazomsajili kiungo wa kati wa klabu ya Calgiari, Nahitan Nandez, ambaye alikuwa akisakwa na Inter Milan, Napoli, Roma na Fiorentina. Klabu hiyo ya Serie A ipo tayari kumuuza mchezaji huyo Januari. ***(Tuttomercatoweb)***

### MBAPPE HAONDOKI PSG

MKURUGENZI wa michezo wa Paris St-Germain, Leonardo amesema haoni kama Kylian Mbappe, 22, ataondoka klabuni hapo mwishoni mwa msimu huu, ingawa nyota huyo bado hajakubali kusaini mkataba mpya. ***(Marca - in Spanish)***

HABARI MICHEZO

## Mguto awafunda waamuzi Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

MWENYEKITI wa Bodi ya Ligi, Steven Mguto, amewataka waamuzi kuchezesha Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2021/22 kwa haki, akitaka timu iliyojiandaa vema ishinde na ambayo haikucheza vema ipate inachostahili ili ijipange upya kwenye mechi zinazofuata.

Akizungumza na waamuzi, wasaidizi na makamisaa wanaochezesha Ligi Kuu msimu wa 2021/22, Mguto ambaye ni Makamu wa Pili wa Rais wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), anategemea kuwa Ligi Kuu msimu huu itakuwa ya nguvu zaidi, hivyo waamuzi wawe makini ili timu zitakazoshinda ziwe ni zile ambazo zimestahili kwa kujiandaa na kucheza vema na si kwa matakwa ya waamuzi.

"Si vizuri mtu anatayarisha timu yake kwa pesa nyingi, halafu anakuja kukosa matokeo mazuri kwa ajili ya mtu mmoja tu, kisa amependa tu. Mimi siamini kama mnapewa pesa, ila wakati mwingine mnapitiwa, au mapenzi ya upande fulani yamezidi, ndiyo vitu kama hivi vinajitokeza," alisema Mguto.

## Usiku Wafia Dansi kuhamia Arusha

**Na Sabato Kasika**

BENDI tatu na vikundi mbalimbali vya burudani, vinatarajia kushiriki kwenye onyesho maalum lililopewa jina la 'Usiku wa Wafia Dansi', litakalofanyika Septemba 25, mwaka huu, jijini Arusha.

Bendi hizo ni Waluguru Original ya mjini Morogoro inayoongozwa na Killer Boy, Bogoss Musica ya jijini Dar es Salaam chini ya Nyoshi el Saadat na Mjengoni Classic ya jijini Arusha inayoongozwa na Digital Mukongya.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, mratibu wa onyesho hilo, Bernad James alisema, huo ni mwendelezo wa kufufua muziki wa dansi nchini ili uwe juu kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

# KOCHA BIASHARA UNITED AGEUKIA WASHAMBULIAJI

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Biashara United, Patrick Odhiambo, amesema kazi kubwa anaoifanya kwa sasa ni kuimarisha safu yake ya ushambuliaji kuelekea mechi yao dhidi ya FC Dikhil ya Djibouti, itakayopigwa Jumamosi wiki hii katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Biashara United wanaoiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika wataikaribisha FC Dikhil Jumamosi wakiwa na faida ya bao moja mkononi baada ya mechi ya awali ugenini kushinda 1-0.**

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kocha Onyango alisema pamoja na kupata ushindi wa bao 1-0, kwenye mechi ya kwanza, walitengeneza nafasi nyingi, lakini washambuliaji hawakuwa makini kuzitumia.

Alisema wana kazi kubwa katika mchezo huo wa marudiano kwa sababu wapinzani wao ni wazuri na mara kwa mara walikuwa wakifika katika eneo lao la hatari kwenye mchezo uliopita, hivyo anapaswa kuwapiga washambuliaji wake msasa ili kuhakikisha wanatumia vema nafasi wanazozipata.

"Ni kweli tulipata ushindi wa bao 1-0 ugenini, ni jambo kubwa na la kuwapongeza wachezaji wangu, lakini katika mechi ya kwanza tulitengeneza nafasi nyingi za wazi hatukuweza kuzitumia vizuri.

"Tumeliona hilo kama benchi la ufundi, hivyo nimeanza kufanyia kazi kwenye hilo [eneo] pamoja na sehemu zingine," alisema Odhiambo.

Alisema baada ya kurejea nchini wakitokea Djibouti, kazi kubwa ambayo anaifanya ni kutoa maelekezo na mbinu katika safu ya ushambuliaji hasa katika suala la umakini wanapokuwa katika nafasi ya kufunga.

"FC Dikhil si wabaya, wako vizuri ukiangalia katika mechi ya kwanza walifika sana sehemu yetu, hivyo mechi yetu ya Jumamosi tunatakiwa kuwa makini sana na kutumia vizuri uwanja wa nyumbani," alisema Odhiambo.

Alisema mpira wa miguu hautabiriki na hauna ugenini wala nyumbani, lakini kulingana na maandalizi wanaoyafanya ana matarajio makubwa ya kupata ushindi mnono Jumamosi. Endapo Biashara United itasonga mbele itakutana na mshindi wa jumla kati ya Hay Al Wadi FC ya Sudan au Al-Ahli SC ya Libya.




Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (wapili kushoto) na Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Straton Chilongola (wapili kulia) wakionyesha jezi pamoja na wafanyakazi wengine wa NMB Tawi la Mbeya jana, wakati wa kukabidhiana vifaa mbalimbali vya michezo. **PICHA: NEBART MSOKWA**. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *NMB yamwaga vifaa vya michezo Mbeya*

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BENKI ya NMB imeikabidhi Serikali ya Mkoa wa Mbeya msaada wa vifaa mbalimbali vya michezo kwa ajili ya kuendeleza soka mkoani hapa hususan katika uendeshaji ligi mbalimbali zinazobuniwa kwa ajili ya kuibua vipaji vya vijana.

Vifaa vilivyotolewa na benki hiyo ni mipira nane na seti nane za jezi ambazo zilikabidhiwa kwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera na Meneja wa NMB Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Straton Chilongola.

Chilongola alisema walitoa vifaa hivyo kutokana na maombi ya Homera ambaye aliviomba kwa ajili ya kuendesha ligi maalumu iliyoanzishwa na Serikali ya Mkoa huo ikijulikana kama Mbeya Super Cup, ambayo ilifikia tamati mwishoni mwa Agosti mwaka huu.

Alisema pamoja na kwamba mashindano kusudiwa yameshapita, lakini benki hiyo iliamua kutoa vifaa hivyo kwa ajili ya mashindano mengine yatakayoanzishwa.

"Vifaa hivi vyote kwa ujumla vina thamani ya Sh. milioni 3.7 na tunaamini wewe mkuu wa mkoa kwa sababu unabuni mashindano mbalimbali, vifaa hivi vitasaidia," alisema Chilongola.

Alisema benki hiyo itaendelea kushirikiana na serikali ya mkoa huo kwenye uendelezaji wa michezo mbalimbali ikiwamo ya kuibua vipaji kwa vijana.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Homera aliushukuru uongozi wa benki hiyo kwa msaada wa vifaa hivyo, akieleza kuwa vitasaidia kuinua sekta ya michezo katika mkoa wake. Alisema michezo hiyo itasaidia kuboresha afya za wananchi wa Mkoa wa Mbeya hasa vijana ambao baadhi yao ni wateja wa benki hiyo.

"Binafsi nashukuru sana Benki ya NMB kwa msaada wa vifaa hivi na nakuomba meneja unifikishie salamu kwa mkurugenzi mkuu wa benki hii maana mmekuwa wadau wetu wazuri sana," alisema Homera.

Mbali na mashindano ya Mbeya Super Cup 2021, ambayo yalifikia tamati mwishoni mwa Agosti, pia Homera kwa kushirikiana na viongozi wa Chama cha Mpira wa Miguu Mkoa wa Mbeya (MREFA), walianzisha Ligi ya Mbeya Pre Season Cocoa Cup 2021 ambayo inashirikisha klabu zinazoshiriki Ligi Kuu na Ligi Daraja la Kwanza.

# Michezo

Alhamisi Septemba 16, 2021

Nipashe




Ronaldo alalama Man U kupoteza Uefa UKURASA 22

PUMZIKA KWA AMANI...



Mashabiki wa Simba, wadau wa soka, viongozi wa dini, ndugu, jamaa na marafiki wakishiriki safari ya mwisho ya kuupumzisha katika nyumba ya milele mwili wa aliyekuwa Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba na mdau mkubwa wa mpira wa miguu nchini, Zacharia Hans Poppe, katika mazishi yaliyofanyika makaburi ya Makanyagio mjini Iringa jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Gomes akiri mafanikio makubwa kambi Simba

●●● Asema tayari amepata muunganiko wa kikosi chake, mamia wamzika Hans Poppe...

**Na Saada Akida**

WAKATI Kikosi cha Simba kikitarajia kurejea Dar es Salaam kesho, Ijumaa, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Didier Gomes amekiri kupata mafanikio makubwa katika kutekeleza programu yake ya mazoezi wakiwa kambini kuanzia ile ya nchini Morocco hadi Arusha walipo kwa sasa.

Simba ilianzia kuweka kambi nchini Morocco kujiandaa na msimu mpya wa 2021/22, kabla ya kuihamishia jijini Arusha kutokana na wachezaji wake wengi kuitwa timu zao za taifa, ambapo sasa itarejea kesho tayari kwa tamasha lao la kila mwaka la Simba Day, litakalofanyika katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumapili wiki hii.

Akizungumza na gazeti hili jana, kocha huyo alisema baada ya kukamilisha usajili wa wachezaji wapya na timu kuingia kambini, aliomba kupatiwa mechi nyingi za kirafiki kwa ajili ya kuiandaa timu yake, jambo ambalo viongozi walifanikiwa kumpatia, hivyo kumfanya apate taswira ya kikosi chake pamoja na kujenga utimamu wa mwili kwa wachezaji.

"Tumekuwa na mchanganyiko wa wachezaji wapya waliosajiliwa msimu huu na ulioisha, nilihitaji kupata mechi za kirafiki, zimenisaidia kuona wachezaji wote wanakuwa na utimamu wa mwili.

"Kwa asilimia kubwa mechi zimenisaidia kwa sababu wachezaji wangu wamepata maandalizi mazuri na kupata muunganiko wa wachezaji wangu wapya na waliokuwapo msimu ulioisha," alisema Gomes.

Ikiwa kambini Simba imecheza jumla ya mechi tano za kirafiki, tatu za kimataifa ambapo mbili ilicheza ikiwa Morocco na timu za huko kabla ya kucheza tatu ikiwa jijini Arusha dhidi ya Castal Union, Fountain Gate FC na kuhitimisha dhidi ya Aigle Noir ya Burundi.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu Bara na Kombe la FA, watacheza mechi nyingine ya kirafiki dhidi ya TP Mazembe ya DR Congo, mchezo utakaopigwa Jumapili katika Uwanja wa Mkapa ikiwa ndiyo siku ya tamasha lao la Simba Day.

Kwa upande wa Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano ya Simba, Ezekiel Kamwaga, alisema kambi awamu ya pili imemalizika na Ijumaa, kesho kikosi kitarejea Dar es Salaam tayari kwa ajili ya Tamasha la Simba Day, Jumapili.

"Tumemaliza 'Pre-season' ya awamu ya pili na sasa akili ziko katika Tamasha la Simba Day, kutakuwa na mechi ya kirafiki dhidi ya TP Mazembe ya DR Congo wakitarajiwa kutua nchini Jumamosi (keshokutwa)," alisema Kamwaga.

Alisema Simba msimu huu imejipanga vizuri na kuanzia kwenye usajili, ambapo wameimarisha kikosi chao zaidi ya misimu uliyopita.

"Malengo makubwa msimu huu ni kuendeleza pale tulipoishia kuanza kuchukuwa ubingwa wa Ngao ya Jamii na makombe mengine yaliyopo mbele yetu kwa kucheza nusu fainali ya michuano ya kimataifa," alisema Kamwaga.

Kuhusu Tamasha la Simba Day, alisema maandalizi yako vizuri na tayari taratibu zingine zinaendelea kufanyiwa kazi ikiwamo suala la tiketi ambapo hadi Jumanne wiki hii tiketi za Sh. 200,000 (Platinum) zilikuwa zimeisha.

"Mauzo ya tiketi yanaenda vizuri tiketi zilizobaki ni VIP A, B, C na mzunguko, mashabiki na wadau wa Simba wanatakiwa kujitokeza kununua tiketi mapema ili Jumapili asubuhi tu wawepo uwanjani," alisema Kamwaga.

Katika hatua nyingine, umati wa mashabiki wa Simba, Yanga na wadau mbalimbali wa soka nchini ulijitokeza kwa wiki kushiriki mazishi ya aliyekuwa Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya klabu hiyo, Zacharia Hans Poppe yaliyofanyika jana katika makaburi ya Makanyagio mjini Iringa.

## Nabi agongewa 'misumari' Yanga

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga ni kama imemgongelea 'misumari' Kocha Mkuu wao, Nasreddine Nabi, ya kuendelea kuwa imara katika kazi yake ya kukiimarisha kikosi chao baada ya kueleza bado ina imani kubwa na Mtunisia huyo huku ikikanusha vikali taarifa za kutaka kumtimua.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli, amesema kocha Nabi yupo mazoezini kama kawaida, na hakuna kitu kama hicho ambacho kinasambaa kwenye mitandao ya kijamii na huenda lengo ni kuwaondoa kwenye mechi yao ya marudiano dhidi ya Rivers United nchini Nigeria.

"Siwezi kuongelea tetesi ambazo zinakwenda kututoa kwenye mchezo wetu wa marudiano. Kama ingekuwa ni kweli basi tungekuwa tumeweka kwenye mitandao yetu rasmi ya kijamii. Mimi nipo, Haji Manara yupo, tungekuwa tumeshaliongelea, lakini kwa sababu halipo, hatuwezi kuliongelea," alisema Bumbuli.

Alisema Yanga imepoteza mechi mmoja tu, lakini haijapoteza mashindano, hivyo hawaamini kama kuna jambo baya lolote ambalo limefanyika la kuweza kumpa mechi mbili au kumwondoa.

"Kwa maana hiyo, kocha Nabi bado yupo yupo sana. Huwezi kumpima kocha kwa mechi moja, labda mechi tatu mpaka nne, ndiyo mnaweza kusema kuwa mbona kama tunapotea kwenye malengo yetu. Nawataka wanachama na mashabiki wa Yanga kuzipuuza tetesi hizo kwa sababu ndizo zina lengo la kutuondoa kuangalia zaidi mchezo wetu wa marudiano," alisema.

Jumapili iliyopita Yanga ilichapwa bao 1-0 kwenye mechi ya hatua ya awali, Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >